# *Kuvaa Silaha Zote Za Mungu*

Asante, Ndugu Borders.

Na hebu tuinamishe mioyo yetu, kwa muda kidogo tu sasa, kwa maombi mafupi.

2 Baba wa Mbinguni, kama vile katika miaka hii mingi, wimbo huo, nimeusikia ukiniita jukwaani kote ulimwenguni, lugha za kila namna. Ninakushukuru, Bwana, ya kwamba mambo yote yanawezekana.

3 Tunaweza kuwazia kuwaona wale wanafunzi kule chini ya mlima wameshindwa kabisa, baada ya Wewe kuwapa uwezo wa kuponya wagonjwa, na kufufua wafu, na kutoa pepo. Nao hao hapo, kabisa, wameshindwa kabisa na ugonjwa wa kifafa, lakini Bwana wa imani akaja akishuka chini ubavuni mwa kilima. Yule baba, akimkimbilia, kasema, "Bwana, mrehemu mtoto wangu, yuna pepo, na mara nyingi yeye huanguka motoni na kuteseka vibaya. Na," kasema, "nilimleta kwa wanafunzi, wala hawakuweza kumponya."

4 Nasi tunaweza kuona, huku upepo unapulizia kidogo na nywele Zake zikipeperuka, Akasema, "Ninaweza, kama ukiamini, kwa kuwa mambo yote yanawezekana kwao waaminio."

5 Na Baba, ni kweli hata leo, ya kwamba mambo yote yanawezekana wakati mashaka yote yanaweza kuondolewa, ndipo imani inaweza kuchukua mahali pake. Na jalia sisi kwa namna fulani, leo hii, kwa nguvu za Mwenyezi Mungu, tuweze kufanya hivyo, tuweke kando kila uvuli wa mashaka na mambo yote ambayo. . . yawezekane kwetu.

6 Tunakushukuru kwa ajili ya mkutano mkuu, kwa ajili ya wahudumu, kwa ajili ya makanisa yao, watu, ushirikiano wao, kwa ajili ya huu ukumbi wa mikutano, kila kitu ambacho kimefanywa, Bwana, tunakushukuru kwa ajili yake. Juhudi zetu zote, tunaomba, Baba, ambazo kila mmoja ametoa zitabarikiwa na kuzidishwa. Na irudi Kwako kama mkate juu ya maji, ukitusamehe dhambi zetu zote na kutuponya magonjwa yetu, na kutusaidia kuishi hivi kwamba, katika ulimwengu huu wa sasa, hata watu wanaweza kumwona Kristo ndani yetu.

7 Zipo hapa leo, leso nyingi zimewekwa jukwaani, kwenye mimbara hii, ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utabariki kila moja yazo, zinawakilisha wagonjwa, wanaoteseka. Nami naomba ya kwamba Roho Mtakatifu, aliyepo sasa, atabariki

leso hizi kwa kusudi zilizokusudiwa. Ulimwangalia kila mmoja, Bwana, ukaweka moyoni mwao kuziweka hapa juu, Ulijua kile walichohitaji, nami ninakushukuru kwa ajili ya watu hao kuwa na imani kiasi hicho, Bwana.

8 Sasa, ninatoa maombi yangu juu ya madhabahu pamoja na yao, na kuomba ya kwamba, katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba utamponya kila mmoja wao, Bwana, kutoka kwa aliye mdogo sana hadi kwa aliye mkubwa zaidi, kutoka—kutoka kwa aliye mahututi hadi kwa aliye mzima sana. Tujalie, Bwana. Jalia lifanyike kwa nguvu za Kristo, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

9 Mwaweza. . .mnaweza kuketi. Na—napungukiwa na maneno inapofikia kusema jinsi ninavyothamini wakati huu wa ushirika hapa Santa Maria. Ninashukuru sana kwa kundi hili la wahudumu ambao wameudhamini mpango huu. Nami ninawathamini, kwa kujua ya kwamba katika madhehebu yao mbalimbali na kadhalika waliyo nayo, kunileta hapa, wamenyoosha shingo zao kabisa, wakainama kinyumenyume kufanya mambo kama hayo, kwa sababu nimeshtakiwa kuwa nayapiga vita madhehebu, na hiyo si kweli, iko mbali na ukweli. Sina neno dhidi ya dhehebu lolote, hata kidogo, bali mfumo wa kimadhehebu siuamini. Mnaona? Ni—ninawaamini watu walio katika madhehebu hayo.

10 Kwa mfano, kama nilikuona ukiteremka kwenye mto mwepesi kwa mtumbwi mdogo, nami nilijua mtumbwi huo ungetumbukia hapa baada ya kitambo kidogo, wala usingeweza kustahimili mawimbi hayo, ningekuwa mtu katili, ningekuwa a—adui kwako kukuacha uelee moja kwa moja kupitia kwenye hayo mawimbi, na nisikuonye, utoke kwenye mtumbwi huo. Unaona? Si—si kwamba nina neno dhidi yako, ni ule mtumbwi ulio ndani yake, jambo ndilo hilo, unaona. Na—nawapenda, nina—ninajaribu kuwasaidia.

11 Na watu hawa wanajua hilo, nao—nao wamenyosha shingo zao, kama tusemavyo, huko mbali na kuegemea nyuma kunileta hapa. Nami nitaninii. . .Kuuweka Ujumbe rahisi tu niwezavyo, michezo midogo ya kuigiza na kadhalika, na, kujaribu kuwa baraka kwenu nyote.

12 Nami nina hakika katika kuondoka hapa, ninachukua baraka kutokana na kuwa pamoja nanyi. Imekuwa ni msisimko mkubwa moyoni mwangu kuona kwamba bado kuna watu duniani, hata baada ya uamsho kwisha, ambao wangali wanajaribu kukaza mwendo kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Nami ninawathamini watu wa aina hiyo, nami. . .nanyi watu. (Nadhani madeni yote yalililipwa, kila kitu?) Gharama zote zililipiwa. Iliwabidi kudhamini hizo, iliwabidi kuzilipia. Laiti ningaliweza kuilipia mwenyewe, bali si—siwezi kufanya hivyo,

siwezi kumudu, sina pesa kama hizo, nami . . . Sababu ya mimi kuja kwenye mikutano midogo, kama nilivyoeleza.

13 Sasa, kuna baadhi ya ndugu zetu, kama vile Ndugu Roberts, na wengi wa watu hao, ambao wana biashara kubwa, nao wana redio na televisheni, na kadhalika, ambao hawana budi kupata maelfu *kadhaa* ya dola kila siku kuidhamini hiyo. Mnaona? Hawana budi kuzipata.

14 Vema, Bwana sikuzote anajua anachofanya. Mnaona? Alijua—alijua kutoniweka kwenye kitu kama hicho, kingenitia kichaa. Mnaona? Ni—nisingeweza kufanya hivyo, kamwe sina nguvu za kiakili za kufanya hivyo, na . . . Lakini Yeye aliniruhusu kuwa na watu wanaonipenda, nami—nami ninajaribu kuchukua kidogo nilicho nacho ili kuweka sehemu yangu katika Ufalme.

15 Sasa, Ndugu Roberts, na Ndugu Allen, na hao ndugu wengine wote walio na hiyo mikutano mikuu, sote tunafanya kazi kwa ajili ya Ufalme mmoja, mnaona. Mnaona? Sisi sote tukifanya kazi kwa ajili ya mahali pamoja. Na kila mtu anajaribu kwa karama zake, ambazo Mungu amempa, kuwaingiza watu katika Ufalme huo.

16 Vema, kwa sehemu yangu ndogo, ninajaribu sehemu yangu kuweka pamoja na yao kusukuma kuelekea kwa Baba, wala si lazima niwe na kitu ila tu gha—gharama, mkutano, watu. Ningeufanyia makanisani, nilikuwa nikifanya hivyo mpaka ikawa ya kuhuzunisha sana, katika nchi za baridi na za joto, huku watu wakisimama karibu na makanisa, watoto wadogo wagonjwa wapate kuombewa, na wake, na wavunjike mioyo. Kwa hiyo basi tukaanza kuwaacha wakodishe kumbi za mikutano na kuwaacha tu watu wazilipie, hilo limechukuliwa, ni hayo tu, limetosha.

17 Nami ni—ninashukuru sana kwa ajili ya watu wenye uwezo walio na mikutano mikubwa na kadhalika, Ninashukuru sana kwa ajili ya watu hao. Hapa siku moja nilisimama karibu na Ndugu Roberts. Mmoja wa waliofanikiwa sana katika mstari huo na katika . . . huko nje hudumani siku hizi, nadhani, ni Ndugu Oral Roberts, ndugu mzuri Mkristo. Nami ndio kwanza niwe kwa Ndugu Tommy Osborn. Na hao ndugu wote wawili waliingia hudumani kwa kuhudhuria mmoja wa mikutano yetu tulipoanza kwa mara ya kwanza. Na ndipo mimi . . .

18 Naye Tommy Osborn, mtu yeyote anamjua ndugu huyo wa thamani, yeye—yeye ni mmoja tu wa watu walio bora sana kule . . . yeye ni kipenzi tu. Nami nimekuwa huko kwake na kuona shughuli yake kubwa kwa ajili ya Bwana na kuona vitabu vyake, na makatibu wake, na IBM kubwa kubwa.

19 Kisha nikaenda kwa Oral basi, nami nikapitia kwenye jengo hilo kubwa la mamilioni ya dola, jinsi walivyoagiza kutoka nje, na dari yote imefumwa kwa nyaya za alumini, na loo, nilijisikia mchafu kutembea kwenye hizo sakafu za—za mahali hapo, na

hizo ofisi kuu, na kuona mitambo mia tano ama mia sita ya IBM ikifanya kazi. Wala barua hata haziguswi na mikono ya wanadamu, mnaona, zinaingia tu mle ndani, na kupitishwa kwenye mitambo, zinapitishwa, zinafunguliwa, zikapitishwa kwenye mikanda ya kuchukulia, na kupitia huku na kutoka, na kwenda namna *hiyo*. [Ndugu Branham alidata vidole vyake—Mh.] Kamwe haziguswi na mikono ya wanadamu.

Ndipo nikawazia, "Jamani, jamani, ni mfumo wa jinsi gani!"

20 Kisha wakaweka...Kulikuwako na baadhi ya marafiki zangu wakingojea nje upande wa mbele. Ndipo lile genge kubwa likakusanyika pale, nami nisingeweza kutokea upande wa mbele, iliwabidi kunitolea upande wa nyuma. Ndipo nikatoka nje, polisi wawili wakaingia na kunitoa nje, nikaingia kwenye eneo la kuegeshea magari upande ule mwingine, nami nilikuwa nimesimama pale nikiangalia. Hakuna madirisha katika kitu hicho, namna fulani tu ya mwangaza usio wa moja kwa moja, na ni kamilifu jinsi gani! Na kuwaona wakichukua mapumziko ya kahawa pale, na mamia tu na mamia na mamia, nami nikawazia, "Ni heshima jinsi gani kwa imani ya mtu mmoja, maskini mvulana mmoja wa Oklahoma, kwamba Mungu angemjalia kitu kama hicho!" Nikawaza, "Mungu, nakushukuru kwa ajili ya jambo hilo."

21 Nikaangalia kule kwa maskini ndugu mmoja, Tommy Osborn. Niliwazia juu yake, jinsi alivyokuwa kule chini, hapa Salem usiku ule, ama, ilikuwa huko Portland, Oregon, wakati yule mwendawazimu alipokimbia jukwaani na kunipa changamoto (Labda watu hapa walikuwapo wakati hilo lilipotukia.), alikuwa anataka kuniua papo hapo jukwaani. Nami nilikuwa nikinena juu ya imani. Akasema, "Usiku wa leo, nitavunja kila mfupa mwilini mwako, ewe nyoka nyasini," akanitemea mate.

22 Nami ni—nilijua vema kuliko kusema lolote, basi nikangoja tu, ndipo Roho Mtakatifu akasema, "Kwa sababu umempa Roho wa Mungu changamoto, usiku wa leo utaanguka miguuni pangu."

Akasema, "Nitakuonyesha nitaangukia miguu ya nani," ndipo akavuta nyuma ngumi yake kunipiga.

Nami nikasema, "Shetani, toka ndani yake, katika Jina la Yesu." Naye akaanguka kukingama miguu yangu hata akanifinyilia sakafuni.

23 Ndipo Tommy na hao wengine walipoona jambo hilo, alienda nyumbani na kujifungia chumbani, akangojea siku tatu ama nne, kisha akaja nyumbani Indiana, akakimbia kuzunguka gari, jamaa mdogo mwenye wasiwasi, kasema, "Ndugu Branham, unafikiri Mungu amenipa karama ya uponyaji?"

24 Nikasema, "Tommy, itakuwa kwamba mazungumzo hayo juu ya karama za uponyaji yataingizwa sana kwenye uchafu

na matope, mpaka yatakuwa ni mabaya sana. Kutakuwako na umati uliochanganyika sana utakaoenda na hili. Kutakuwako na mihemuko ya kila namna, na itikadi, na mambo ya kila namna yakiibuka, mpaka ikatokea kwamba kila mtu hana budi kuwa na namna fulani ya huduma ya uponyaji la sivyo hata hawatakuwa. . . hawatajisikia wako hudumani. Na hiyo ni kumdhalilisha tu mtu ambaye anajaribu kabisa kushikilia mahali pake. Kumbuka, wewe ni muhimu tu katika Ufalme wa Mungu kama mtu mwingine yeyote." Na kwa hiyo, nami nikasema, "Mungu alikuita kuhubiri Injili, sivyo?"

Akasema, "Naam."

25 Nikasema, "Unaonekana kama kijana mwanamume mwenye matumaini." Nikasema, "Basi, uponyaji wa Kiungu huambatana na kuhubiri Injili." Hiyo ni kweli. "Kwa hiyo waombee tu wagonjwa." Na hivyo ndivyo amefanya. Jinsi Mungu alivyombariki mvulana huyo, mwerevu, mwenye akili!

Nilisimama hapo na kuangalia pande zote, nilijisikia mkubwa *hivyo*, nikisimama pale mbele ya jengo hilo kubwa, nikiangalia kote. Nikawaza, "Jamani!"

26 Kwa namna fulani nikashikwa na hisia ndogo ya kiajabu ikipitia ndani yangu, nami nikawazia juu ya Tommy kule, na Oral hapa, nami niliwatangulia hudumani wote wawili. Na jamani, ningechukia wao kuja ofisini mwangu, taipureta moja ndogo mwishoni mwa trela, nikijaribu kutafuta mtu wa kunisaidia kujibu barua, na kadhalika. Nikawaza, "Jamani, nini. . . hakika ningejionea aibu," na namna hiyo.

27 Nikawazia, "Vema, Mungu, nadhani kwa urahisi tu sikuwa. . . Usingeweza kuniaminisha kiasi hicho, namna hiyo. Huenda, nilifanya jambo ambalo halikuwa sahihi, kwa hiyo labda usingeweza kuniamini. Labda hivyo ndivyo ilivyokuwa."

28 Na sasa, si kuwadhalilisha hao ndugu, ama si. . . Natumaini halisikiki la kukufuru, lakini dhahiri tu kama mnavyoisikia sauti yangu, Sauti ilinena nami, "Lakini," kasema, "Mimi ni Urithi wako."

Nikasema, "Asante, Bwana. Ni—nina furaha kuwa na Urithi huo." Mnaona?

"Mimi ni Urithi wako."

29 Kwa hiyo nikawazia hiyo ni. . . ilikuwa yote. . . ilisikika. . . ilinifanya kujisikia vizuri. Nadhani Yeye alifanya hivyo tu kunitia moyo, kwa sababu nilijisikia kana kwamba sikuwa nimefanya lolote niliposimama na kuyaangalia, yale Mungu alikuwa amewafanyia hao ndugu.

30 Ndipo nikawazia labda mwishoni mwa safari yangu, wakati hatimaye nitakapomaliza mahubiri yangu ya mwisho na kuomba maombi yangu ya mwisho, kwamba labda Yeye atanipa sehemu

ndogo Yake Mwenyewe Huko mahali fulani. Nami natumaini kuwa huko Siku hiyo pamoja nanyi nyote.

31 Ajabu, mvulana mdogo, mvulana mdogo sana, hakuonekana mwenye umri wa zaidi ya miaka kumi na miwili, simwoni hapa, alikuwa na mkanda mdogo wa bawabu mkononi mwake, amekuja sasa hivi tu, na kubisha dirishani. Nilikuwa nimeketi pale nikisoma Maandiko, nilikuwa nikisoma Maandiko ya kuhubiri alasiri ya leo, nami ni—nilikuwa nikiangalia kote kuhakikisha ya kwamba nimeweka Maandiko mahali pazuri. Nami nilikuwa nimeandika machache hapa, nami ni—nilikuwa nikiyachunguza. Ndipo mvulana huyu mdogo akaja, kasema, "Naweza . . . Ndugu Branham, naweza kukupiga picha?"

32 Nami nikasema, "Naam, Bwana, hakika unaweza," nikasema, "kama kamera yako itastahimili." Kwa hiyo nikatoka nje. Akanipiga picha, nikasema, "Afadhali uichunguze, huenda imeharibika." Naye akacheka tu, maskini jamaa wa kuvutia.

Naye akasema—akasema, "Sidhani imeharibika."

Nami nikasema, "Vema, natumaini haijaharibika." Ndipo akageuka na kuniangalia. Nikasema, "Unaishi hapa?"

Akasema, "Naam."

Nikasema, "Hakika mna hali nzuri sana ya hewa zaidi ya mahali popote nilipowahi kuwa."

33 Naye akasema, "Asante." Akasema, "Vema, Ndugu Branham, sitaki kukuweka, ninajua unasoma, nisipokutana na wewe hapa tena, nitakutana nawe Ng'ambo ya pili." Mvulana mdogo, akiwa na . . . maskini bawabu mdogo.

Nikawaza, "Hiyo ni kweli." Naam.

> Kutengana, huacha nyuma yetu
> Kumbukumbu za kudumu;
>
> Kumbukumbu, ambazo labda mwingine,
> Wakati akiabiri bahari adhimu ya maisha,
> Ndugu mpweke ambaye chombo kimemwendea mrama,
> Akiona, atatiwa moyo tena.

34 Hiyo ni kweli. Hebu na tuone mahali tunapoweza kutoka, na kuweka nyayo, kwamba kama kuna kesho, wale watakaokuja watafuata hizo nyayo. Hebu na tuhakikishe zinaongoza moja kwa moja hadi Kalvari, maana hapo ndipo mahali. Asanteni nyote tena.

35 Na sasa, huenda kusiwe na, ninii . . . Sijui ni nani anayeshughulikia ghala hili la silaha, kama ni a—afisa wa zamu, ama kama ni nanii . . . yule aliye, ama—ama kama ni kamati, ama yeyote yule, ninataka kuwashukuru kwa ajili ya wakati huu wa thamani ambao wametupa, na jengo hili la jeshi hapa.

36 Wala sijui mengi sana kuhusu jeshi. Daima ni—nilitaka kuwa askari. Mlisikia hadithi ya maisha yangu, jinsi, wakati nilipokuwa tu nikiangalia magazeti na kuwaona askari, nami ni—ni—nilitaka sana kuwa na sare. Nami na—nafikiri ni sifa njema kuwa na. . .kuvaa sare ya Marekani hii, kwa kile tunachowakilisha, heshima kuu. Vita vya Kwanza vya Dunia, nilikuwa mdogo sana, nilikuwa tu na umri wa miaka minne hivi. Na katika Vita vya Dunia vilivyopita, nilikuwa na sura mbaya sana ama kitu kama hicho, hawakunichukua, kwa hiyo hawa—hawangenichukua.

Nikaenda kule kujiandikisha kama mhudumu, naye akasema, "Umeoa?"

Nami nikasema, "Naam, bwana, nimeoa."

Naye akasema, "Tunaweka wahudumu katika daraja la IV-H." Kisha kasema, "Tunapowahitaji tunawaita."

37 Nikasema, "Nitakuwa nikingojea, Bwana. Hakika ningetaka kwenda huko nje na kuwatia moyo hao wavulana, nifanye yote niwezayo." Kamwe hawakuniita, kwa hiyo nadhani ha—hawakunihitaji.

38 Kwa hiyo nakumbuka nilitaka sana kuvaa sare, mimi. . . jamaa fulani alikuwa na suti ya Skauti, nami nikamwambia, "Je, utakapoichakaza, utanipa?" Naye akasema atanipa. Na hatimaye, miaka miwili au mitatu ikapita, nami nikaendelea kuulizia suti hiyo, basi akajaribu kuitafuta, naye hakupata kitu ila soksi ndefu ya mguu mmoja, nami nikaichukua hiyo, nikaivaa hiyo, hiyo soksi ndefu ya mguu mmoja. Basi ni—ningesimama ubaoni shuleni kuandika, nami ningeivaa hiyo soksi ndefu kwenye mguu wa kulia, ili niweze kusimama *hivi*, mwajua, na kuandika kwa upande. Kila mtu alidhani nilikuwa na mbili, mwajua, nilikuwa tu na hiyo moja, kwa hiyo ilikuwa ni sare. Lakini sikuzote kwa namna fulani nilikuwa mdogo, na. . .

39 Mnajua, hata hivyo kweli ni—nilipata sare, huenda msiione kwa nje, lakini iko upande wa ndani kwa kuwa. . . Nitazungumza juu ya hiyo katika dakika chache tu. Nami natumaini ya kwamba ninaweza kuishi ili ionekane kwa nje, ndilo ombi langu.

40 Hebu na tusome sasa kutoka katika Maandiko, mlango wa 6 wa Waefeso, kifungu cha 10 kuanzia:

> *Hatimaye, ndugu zangu, mzidi kuwa hodari katika Bwana,. . .katika uweza wa nguvu zake.*
>
> Mkivaa *silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za shetani.*
>
> *Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme, na mamlaka, juu ya wakuu wa. . .giza la dunia hii, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.*

*Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama.*

*Basi simameni, hali* mmejifunga *kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani;*

*Na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani;*

Na *zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani,* ambapo *kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu.*

*Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa . . .* imani, *ambao ni neno la Mungu.*

41 Jeshi la Marekani halikunipokea kwa sababu, nadhani, kulikuwa na watu waliostahili zaidi. Lakini nina furaha kwamba niliandikishwa katika jeshi moja, la Bwana, Naye akanipa sare.

42 Paulo hapa anazungumza, anazungumza kuhusu kumwandaa askari kwa ajili ya vita. Injili ina mielekeo mingi, unaweza kuifananisha na kitu kimoja au kingine. Naye Paulo ananena habari zake kama mkimbiaji, katika Waebrania mlango wa 12, "Kwa kuwa tumezungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi, ituzingayo kwa upesi." Anazungumza pale juu ya Olimpiki, au labda Sarakasi ya Kirumi. Na kwa hiyo sasa anazungumza juu ya watu wenye silaha wakienda vitani na jinsi anavyopaswa kujiandaa.

43 Nami nilikuwa nikiwazia, alasiri ya leo, kwa kuwa tunafunga hapa katika ghala hili la silaha leo, kwamba ningechukua hilo kama somo: *Kuvaa Silaha Zote za Mungu*. Mjivike silaha, mwe tayari, kwa maana kushindana kwetu si juu ya damu na nyama, bali dhidi ya Shetani, adui wa Mungu, falme, na uovu, na pepo wachafu, uovu katika ulimwengu wa roho. Nasi tunakaza mwendo kuelekea kwenye mede ya wito mkuu, na bila shaka tuko vitani.

44 Wala hakuna taifa lingethubutu kumtuma mtu kwenye uwanja wa vita, asiyefunzwa. Huenda akafanya si auawe tu yeye mwenyewe bali na kundi lingine pia, hajui jinsi ya kushikilia, na kwa hiyo lazima aandaliwe kwa ajili yake. Nayo mataifa yanajua hilo vizuri, yanawatayarisha watu wao.

45 Sasa, mfumo wa kijasusi wa ulimwengu mzima, mwajua, ni kwamba hata ingawa tuna urafiki na mataifa mengine kama Uingereza na—na marafiki ze—zetu, hata hivyo tuna majasusi huko Uingereza, na Uingereza ina majasusi hapa. Nasi tuna majasusi kote ulimwenguni, nao ulimwengu una majasusi hapa, kama tuna urafiki ama hatuna urafiki, ndio mfumo

wanaoutumia. Inaonekana tu kwamba wewe, katika jambo hilo la kitaifa, huwezi kuamini chochote.

46 Nanyi mnajua ni kwa nini? Ni kwa sababu ulimwengu mzima unatawaliwa na Shetani. Kila ufalme ulimwenguni unatawaliwa na Shetani. Tunachukia kuwazia hilo, bali hilo ni Maandiko. Mnajua, adui alimpeleka Bwana wetu juu ya mlima mrefu, mrefu sana, mrefu mno, na kumwonyesha falme zote za ulimwengu, na kusema, "Zote ni zangu, mimi ndiye mtawala wake. Ninazifanyia lolote nitakalo, nami nitakupa hizo."

47 Angalia hekima ya Bwana Yesu ikidumu na Neno la Mungu. Alijua angezirithi kwenye ule Ufalme, katika Ufalme ujao katika ule Utawala wa Miaka Elfu Moja, kwa hiyo Yeye akasema, "Nenda zako, Shetani."

48 Sasa, mnaona, Shetani anaweza kufanya nazo lolote atakalo. Sasa, kama mataifa haya yangaliongozwa na Mungu, tusingekuwa na vita, kusingekuwako na mapambano tena, hapo. . . ungekuwa ni wa Mungu. Lakini Shetani ndiye mtawala wa kila ufalme, anautawala ulimwengu. Lakini siku moja. . .

49 Unaweza kuliona katika watu. Kila mtu anataka taifa moja liutawale ulimwengu, wanataka bendera moja, nao wanataka kuwa taifa lenye nguvu kuliko yote ulimwenguni mwote, na kuchukua kila kitu chini ya mamlaka yao wenyewe, na kufanya mataifa mengine yote kuzungumza lugha yao. Ni kitu gani? Ni ninii tu, inaonyesha ya kwamba kuna mahali kama hapo.

50 Kama Daudi alivyosema, "Kilindi kinapoita kilindi. . ." Sasa, kabla hapajakuwapo na kilindi cha, ama, kuita kwa ndani, hapana budi kuwe na kilindi cha kuitikia wito huo. Kwa maneno mengine, mara nyingi nimetoa tamshi la namna hii katika kusema hivi, nikiyanukuu Maandiko haya: Kabla hapajakuwapo na ua la kukua ardhini, ilibidi kuwe na ardhi kwanza, kabla hapajakuwapo na ua la kukua ardhini.

51 Hebu nenda hapa nje kwenye ufuo wa bahari na kuwazia juu ya samaki. Sasa, kabla hapajakuwapo na pezi mgongoni mwa samaki, ilibidi kuwe na maji kwa ajili yake kuogelea apate kutumia hiyo pezi, kabla pezi hilo halijakuja pale. Unaona?

52 Na sasa, sote tunatazamia Mahali ambapo hapana mauti, ambapo hapana maradhi. Tuangalieni: Kama wavulana wadogo na wasichana wadogo ilikuwa, kusudi letu muhimu lilikuwa ni kushinda gololi kadhaa, au kubingirisha vifuniko, ama kucheza na wanasesere. Kisha ikatubidi kwenda shuleni. Ndipo wakati tuliponinii. . .Jambo lingine lilikuwa ni tumchague mwanamke yupi, ama mwanamume yupi, kama mwenzi wetu wa maisha. Ndipo familia ikaja, wao—wao, familia, haina budi kuelimishwa, nyumba haina budi kulipiwa. Na ifikapo wakati hayo yamekamilika, tumekwisha pia, nywele zetu zimeingia mvi na kunyonyoka, na sisi ni. . . uso wetu unaelekezwa kwenye

machweo ya jua, mnaona, bali tunatamani *kitu* hicho fulani ndani yetu, kinachosema pale, kwamba kuna Mahali fulani.

53 Ni kitu gani? Inaonyesha ya kwamba Mahali hapo pako mahali fulani. Wewe huyu hapa umeketi hapa alasiri ya leo. Niliangalia, nikapita karibu na mama mmoja, Roho Mtakatifu akasema tu, "Geuka." Alikuwa ameketi pale kwenye kiti cha magurudumu huku ameinua mkono wake. Anafanya nini hapa? Huyu hapa msichana mrembo, ameketi hapa, amelemaa; labda mwanamume ameketi hapa, yabisi kavu; labda mmoja aliye na ugonjwa wa moyo.

54 Sasa, watu hawa kwenye kiti cha magurudumu wanaweza kuishi maisha ya kawaida. Mnaona, mara nyingi mnashangaa wakati mwingine kuhusu walemavu. Mtu yeyote anaweza kuona wao ni walemavu, hakuna mwujiza katika kuwaambia wao ni walemavu. Ni huyu anayeonekana mzuri na mwenye afya, kisha kuwaambia mahali ilipo shida yao, huo ndio mwujiza.

55 Lakini wakati mwingine mtu anapokuwa mlemavu wanafikiri huo ndio mwisho wake. Loo, la, la. Angalieni tu. Na—najua ni kitu gani, bali ninaangalia nione kile Yeye anachoniambia nifanye. Mnaona? Ninaweza tu kuzungumza anapozungumza Yeye. Lakini mnaona, wana—wana kiu, wana njaa ya mahali fulani. Kitu fulani kinawaambia ya kwamba kuna mamlaka mahali fulani yanayoweza kuwakomboa. Vema, hakika tu kama hilo lilivyo moyoni mwako, ukiwazia hilo, hapana budi kuwe na chemchemi, mahali fulani, ya uponyaji. Mnaona? Mnaona? Mnaona?

56 Kabla hapajakuwepo na uumbaji, hapana budi pawe na Muumba wa kuumba huo uumbaji. Unaona? Na maadamu ndani yako una kiu ya kutaka mahali fulani pa kugusa, kuna ninii, hakika chemchemi iliyofunguliwa mahali fulani ambapo unaweza kugusa, kwa sababu haina budi kuwa, Kitu fulani kimeumba hicho ndani yako. Na ni . . . kama hakukuwa na Biblia ya kutwambia hivyo, bado ingebidi iwe ni uhalisi, kwa sababu kuna kitu fulani ndani yako ambacho Muumba ameumba. Na kabla ya kuweza kuwa na shauku, hapana budi kuwe na kitu cha kutimiza shauku hiyo.

57 Je, uliwahi kuwa na kitu ulichokuwa ukikionea njaa wala kamwe usingeweza kupata ladha yake? Baada ya kitambo kidogo unakipata, hicho hapo. Mnaona?

58 Sasa, tunatamani mahali fulani ambapo hapana mauti, hapana sononeko, hapana huzuni, hapana uzee, Nchi hiyo iko mahali fulani. Wala kamwe hatutaweza kulifanikisha kwa bunduki, na kupigana, na kadhalika, kwa silaha za asili za kimwili, lakini kuna Nchi ambayo tunaweza kuiendea, na ni vita kufika huko.

59 Wakati Mungu alipowapa Israeli Palestina wakati walipokuwa Misri, lakini iliwabidi kupigania kila inchi yake,

ndipo akamwambia Yoshua, katika Yoshua 1, Yeye alisema, "Kila mahali nyayo za miguu yenu zitakapokanyaga, nimewapa ninyi." Kwa hiyo nyayo za miguu maana yake ni milki. Mnaona, endelea tu kutembea, kutembea, ukikaza mwendo. Na kila mara unapopiga hatua kuingia katika Ufalme wa Mungu, hiyo ni yako, kwenye tu. . . Na mambo yote yanawezekana yaliyotolewa, na yote yaliyotolewa yanawezekana. Lakini ni vita.

60 Na katika mafanikio yetu hapa katika—katika taifa, ya kujaribu kuangalia huku na huku tuone ni kitu gani kinachotukia, majasusi wa mataifa mengine wako hapa, wakitupeleleza, tuna majasusi huko nje wanaotupeleleza. Wanaangalia kuona ni silaha ya namna gani mpya itakayotokea. Na halafu wananinii. . . kuirudisha hiyo nchini mwao, na kutafuta kitu cha kukabiliana na silaha hiyo, kitakachoishinda, itakayokuwa bora zaidi kidogo.

61 Sasa, vita vya kwanza ninavyokumbuka ni Vita vya I vya Dunia, nilikuwa mvulana mdogo. Ninakumbuka baba yangu akipanda barabarani akiendesha farasi wawili na mkokoteni, yeye. . . naye alikuwa na gunia la maharagwe limewekwa kwenye huo mkokoteni. Nasi tungeshuka kwenda Jumamosi na kununua, gunia la maharagwe, na—na gunia la unga, na gunia la posho, na—na vitu vichache namna hiyo kutuendeleza kote katika juma.

62 Nami nikasema. . . Nilimsikia akisema, "Vita vilitangazwa, Mama. Unasikia filimbi hizo zote?" Baba alikuwa na umri wa kama miaka ishirini na mitatu au ishirini na minne wakati huo. Akasema, "Huenda ikanibidi kwenda."

63 Ndipo nikawaza, "Ati baba yangu aende vitani? Nitachukua gunia hili la maharagwe, na kumpiga mtu nalo kama nanii wangu. . . " Mnaona? Nami nilikuwa jamaa mdogo tu. Nami ninakumbuka bunduki yake, ile bunduki ya kale ya Springfield, jinsi alivyosema ingepiga risasi ipitie kwenye nguzo ya simu. Bunduki hiyo imepitwa na wakati kabisa.

64 Injini za kale za mvuke kwenye reli, zilizokuwa zikileta risasi na—na kuwaleta askari kwenye uwanja wa vita, garimoshi hilo lilikuwa ni kitu kikuu cha kale, lakini limepitwa na wakati, hawana hilo tena. Wana kitu bora zaidi kuliko walichokuwa nacho wakati huo.

65 Ndipo katika vita vilivyofuata, bu—bunduki ya Garand ikachukua mahali pa Springfield, na sasa wana makombora ya atomiki, bunduki ya Garand imekwisha. Daima wanafanya upya na kupata kitu bora zaidi ku—kupambana na adui.

66 Nasi ni jeshi, Kanisa la Kikristo ni jeshi la Mungu. Sisi ni askari, askari wa msalaba. Na ni kazi ya kila taifa kuona ya kwamba askari wao wana zilizo bora kuliko zote zilizopo. Hakuna kitu. . .

67 Nami nilikuwa nikihubiri hivi majuzi usiku kuhusu mafanikio kwenye mkutano mwingine mahali fulani, nami nikazungumza kuhusu askari wetu wa Marekani. Wakati Washington ilipokuwa huko Valley Forge, karibu nusu yao walikuwa wamevaa viatu, walikuwa miguu mitupu, lakini walikuwa na jemadari aliyeomba usiku kucha, akavuka Delaware kesho yake. Hiyo ndiyo sababu tuna Marekani. Ni watu, watu hodari waliokuwa na kitu cha kupigania, kamwe hatupaswi kuwaangusha.

68 Sasa, walikuwa na makombora siku hizo, visu, hizo ndizo bora sana walizokuwa nazo. Taifa lolote . . . Walikuwa na kilicho bora zaidi tulichoweza kuwapa. Na siku hizi, angalieni tofauti katika jeshi letu leo na ilivyokuwa wakati huo.

69 Lakini mnajua, wakati Mungu . . . Akiwa asiye na kikomo, asiye na kikomo hawezi kubadilika. Hapo ndipo imani yangu inapotulia, ni juu ya Neno la Mungu, kwa sababu Hilo ni Mungu. Na Mwenyewe . . .

70 Mnaona, Neno ni wazo lililotamkwa. Na wakati Mungu anapowazia chochote kilicho niani Mwake, basi anapokitamka, ni cha Milele. Kwa sababu hakuna mtu aliye bora kuliko neno lake, naye Mungu ni wa Milele, na Neno Lake ni la Milele pamoja Naye, kwa sababu ni sehemu Yake. Nawe u sehemu ya neno lako mwenyewe, na Mungu ni sehemu ya Neno Lake Mwenyewe.

71 Sasa, ninaweza kusema lolote, ama taifa linaweza kusema lolote, katika mwaka mmoja ama miwili inawabidi kuendelea kuliboresha. Lakini Mungu ni mkamilifu, na uamuzi Wake wa kwanza ni . . . Hawezi kuubadilisha tena, kwa sababu ni mkamilifu, maana Mungu asingefanya lolote isipokuwa liwe kamilifu. Kwa hiyo wakati Mungu . . .

72 Vita vya kwanza vilivyopata kupiganwa havikupiganwa duniani, vilipiganwa Mbinguni, Mikaeli na Malaika zake dhidi ya Lusifa. Nao walifukuzwa kutoka Mbinguni, ndipo basi jeshi hilo kuu la ibilisi na pepo wake wote wakaanguka juu ya nchi. Naye Mungu alijua kutakuwako na vita.

73 Nami ninaamini Yeye alijua tangu mwanzo kila kitu ambacho kingepata kuwako. Kama Mungu hana kikomo, Yeye alijua kila kiroboto ambaye angekuwako duniani, kila kisubi, ni mara ngapi angepepesa jicho lake, na ni kiasi gani cha shahamu wote wangetengeneza pamoja. Yeye hana kikomo.

74 Kwa hiyo, Mungu asiye na kikomo, atalichagulia jeshi Lake Silaha bora zaidi ambayo ingetolewa, Naye akaichagua, Nayo ilikuwa ni Neno Lake. Mungu alilipa jeshi Lake Kifaa kilicho bora zaidi ambacho lingeweza kutumia, na daima lingeweza kukitumia, wala kamwe hakingeweza kubadilishwa, wala kamwe hajawahi kukibadilisha tangu wakati huo. Hukiboreshi, kinabaki vile vile wakati wote. Ni Neno la Mungu ambalo aliwakinga watu Wake kwalo.

75 Haidhuru Shetani atapata vitu vingapi, ni vitu vingapi jeshi lingine lolote litapata, ama chochote kile, hakiwezi kamwe kuchukua mahali pa chaguo la kwanza la Mungu, Neno Lake. Yeye aliwapa Neno Lake, ahadi Yake, na kusema, "Dumuni Nalo," bora zaidi ambalo lingeweza kujulikana.

76 Sasa, adui alijua mradi jamii ya binadamu ilidumu na Neno hilo, asingeweza kamwe kuwagusa, (Sasa, ninaanza kujisikia kubarikiwa sasa hivi.), maadamu jamii ya binadamu ilidumu na Neno. Mungu aliimarisha familia Yake duniani, jeshi Lake, katika Ngome ya Neno Lake, hiyo ndiyo Ngome yetu. "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia wakawa salama," wameimarishwa.

77 Bwana ni Neno. Wako Mle ndani wamekingwa na ni salama milele, maadamu jamii ya binadamu inadumu katika Neno. Mradi tu Kanisa linadumu katika Neno, limelindwa, hakuna kitu kitakacholisumbua.

78 Sasa, adui, kujaribu kumleta jasusi mle ndani, kujaribu kuingia mle kwa njia fulani, ilimbidi apate namna fulani ya mbinu apate kuingia. Hivyo ndivyo wapelelezi wanavyoingia katika taifa hili, ni namna fulani ya mbinu ya kupitia kwa ma—mabalozi na kadhalika, inabidi wawe na njia ya kujipenyeza humu ndani. Ilibidi Ukomunisti ufanye jambo lile lile.

79 Tunapowazia juu ya ukomunisti, hebu niwape neno dogo. Hili litasikika la kigeni kwa mhubiri, lakini kamwe usiogope chochote kuhusu ukomunisti, si kitu. Ninataka mhudumu yeyote, ama msomaji yeyote wa Maandiko, anionyeshe kamwe katika Biblia ambapo ukomunisti utautawala ulimwengu. Urumi utautawala ulimwengu, kulingana na Biblia. Usiuangalie huo, usiuwazie ukomunisti, ni kibaraka tu mikononi mwa Mungu kutimiza mapenzi Yake. Yale hasa aliyosema, Yeye hutumia hayo. Lakini kamwe usihofu kuhusu ukomunisti, ni Urumi, Biblia ilisema.

80 Kuna mapazia matatu. Ninapowaacha alasiri ya leo, ninawaachia hili: Kumbukeni, kuna mapazia matatu, mojawapo ya hayo linaitwa pazia la chuma, mojawapo pazia la mwanzi, Uchina na kadhalika, mashariki, halafu kuna pazia la zambarau. Usiogope pazia la mwanzi wala pazia la chuma, bali kuwa mwangalifu na hilo la zambarau.

81 Afadhali mwe waangalifu, mpinga-Kristo atakaribia sana kuwapoteza walio Wateule. . .Wateule ni akina nani? Wakati nuru hiyo inapoangaza juu ya huyo M-w-a-n-a. . .j-u-a likiangaza juu ya mbegu ambayo inaongozwa na uhai wa mimea, itakuwa hai. Na wakati M-w-a-n-a wa Mungu anaiangazia hiyo Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani, itafufuka upesi hivyo, mara tu, sijali ni hali gani ya maisha, huenda ikawa ni kahaba, huenda ikawa ni mlevi ama mcheza kamari, itaangaza dakika

hiyo, mara tu itakapomgusa. "Kuwadanganya walio wateule kama yamkini."

82 Sasa, angalieni, Shetani alijaribu kuingia mle ndani kupeleleza, aone ni nini, jinsi angeweza kuishika jamii hiyo ya binadamu, naye akachukua moja ya mbinu maarufu sana ambazo, vema, ilionyesha ya kwamba ilimpasa awe nguvu za kimbinguni kuliwazia, naye akatumia hii mara ya kwanza na akafanikiwa, naye amefanya hivyo tangu wakati huo, na angali amefanikiwa kufikia kiwango fulani, alitumia hoja dhidi ya imani.

83 Shetani alimjia Hawa na kuanza kutoa hoja dhidi ya Neno la Mungu, ile Silaha kuu ambayo Mungu alikuwa amewakinga nayo watu Wake. Alianza kutumia hoja, "Sasa, ni kweli tu kwamba Mungu asingewaangamiza. Hakika hamtakufa." Lakini kumbukeni, enyi marafiki, hiyo ndiyo mbinu ya Shetani kwanza kabisa, na angali anatumia kitu kile kile, na angali anafanikiwa nacho, kutoa hoja.

84 Wanajaribu kutoa hoja, "Kwa nini tumhitaji Roho Mtakatifu leo hii? Kwa nini tuhitaji uponyaji wa Kiungu? Kwa nini tuhitaji *hili*, na ni vipi tungehitaji Pentekoste nyingine? Sisi sote tumestaarabika." Ndivyo walivyokuwa pia.

85 Lakini mnaona, kama chochote kilichohitajika kwanza kabisa, na chochote Mungu alichowapa kwanza kabisa, hicho ndicho kinachobaki daima. Basi mbinu za kutoa hoja ndizo Shetani alitumia, na hizo ndizo anazotumia daima, kutoa hoja.

86 Tunamjua adui yetu, kwa sababu adui yeyote. . .Sasa, Ndugu zangu, nimeyaondokea Mafundisho, mnaona, hapa, lakini sina budi kusema jambo hili. Adui yeyote anayetoa hoja dhidi ya, ama, mtu yeyote, kanisa lolote, shirika lolote, mtu yeyote anayehoji dhidi ya alama moja ya vituo vya Neno la Mungu ni adui yako. Inahitaji Neno kumshinda adui.

87 Wakati Yesu wa Nazareti alipokuwa hapa duniani Yeye kamwe hakutumia nguvu Zake, hata hivyo Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, kamwe hakutumia nguvu Zake wakati Shetani alipokabiliana Naye, alisema, "Imeandikwa." Ni kitu gani. . .? Ilimbidi kufanya hivyo, kwa sababu Hawa alivunja hilo. Na kile Hawa alichopoteza, Kristo alikirudisha. Mahali ambapo Hawa aliachilia, Kristo alipaimarisha tena. "Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu. Imeandikwa, usimjaribu Bwana Mungu wako." "Imeandikwa, imeandikwa!" Ni kitu gani? Alidumu na ile Mizinga ya asili. Lakini Hawa aliachilia, akaanza kusikiliza hoja.

88 Na kuna watu siku hizi ambao karibu wanaweza kutoa hoja na kuwathibitishia ya kwamba jambo hilo si sahihi. Shetani alifanikiwa sana kwa Hawa. Hoja hufanya nini? Inalifanya liwe la kuvutia. "Vema, sasa, kama nikitaka kuwa wa kidini. . . "

89 Tafadhali msinielewe vibaya sasa. Mtu anafikia mahali anapotaka kuwa. . .anataka dini. Anataka kuokoka, hataki kwenda jehanamu. Hakuna mwanadamu anayetaka kwenda mahali hapo. Haikuandaliwa kwa ajili ya mwanadamu, iliandaliwa kwa ajili ya ibilisi na malaika zake, haikuandaliwa kwa ajili ya mwanadamu. Sasa, lakini mwanadamu hujipeleka mle ndani. Mungu hutupa kila taa nyekundu awezayo kuikingama, nao watu wanapiga vita moja kwa moja wapate kuivuka hiyo.

90 Inakubidi, kabla hujaweza kuwa asiyeamini, inakubidi kuikwepa imani katika Neno la Mungu kwanza, kabla hujaweza kuwa asiyeamini. Inakubidi kuipita taa nyekundu ya Mungu.

91 Angalieni, watu hawa, jinsi ambavyo Shetani alililifanya la kuvutia sana! Nayo dhambi inavutia. Ninajua sina muda mrefu sana kwenye somo hili, lakini ningetaka tu kuchukua muda wangu kwa dakika chache. Hebu tusimame kwa hilo kwa muda kidogo tu. Tungeweza kuwa hapa asubuhi juu ya somo lile lile, lakini hebu tuangalie tu.

92 Dhambi katika siku za mwisho, Petro anatwambia, kwamba atazunguka-zunguka kama simba angurumaye, anazidi kuwa mbaya. Sasa, nataka kuwaulizeni jambo fulani. Mimi sihukumu, ninatoa tu tamshi. Baadhi yenu ninyi wazee, ama hebu tumchukue yeyote wetu, na turudi kwenye picha ya mwanamke fulani miaka hamsini ama sitini iliyopita ambaye alikuwa malkia wa urembo katika siku zake, Pearl White, Scott Jackson, yeye alidhaniwa kuwa mwanamke aliye mrembo kuliko wote Marekani. Kama ungeona picha yake imetundikwa ukutani, ungefikiri ilikuwa ni kitu cha kale. Ni kitu gani? Ni, wanawake wamekuwa warembo zaidi. Shetani anawavalisha hivyo, akiwarembesha hivyo, akihakikisha kuwa hiyo inakuwa hivyo kwa sababu imekuwa ya kuvutia zaidi. Ni ninii . . .

93 A—afadhali niyaondokee hayo, maana niliahidi sitayaingilia mambo hayo tena. Mnaona? Lakini jinsi lilivo, hicho kilikuwa ndicho kifaa chake cha kwanza, anakirudisha moja kwa moja tena katika siku za mwisho. Enyi akina dada, msijichanganyishe katika upuuzi huo, kaeni mbali nao.

94 Je, mliona, katika kila jinsia iliyopo, wa kiume daima ndiye mrembo kuliko wote? Ni nani aliye mrembo sana, kusema ninii. . .katika jamii ya ndege? Mwangalie ma—maskini, mtu fulani alisema kwale, hiyo ni sawa. Hebu tumwangalie jogoo mkubwa wa kwale, jinsi alivyo mrembo, kisha tumwangalie maskini mtetea mwenye madoadoa. Hebu na tuwaangalie kulungu, kulungu jike, maskini kitu cha kawaida, kinachoonekana cha kinyumbani, na kulungu dume, spishi kubwa mno nzuri.

95 Mwangalie fahali na ng'ombe, mwangalie kulungu, wa kiume na wa kike, angalia chochote unachotaka kuangalia, nawe

daima utaona ya kwamba wa kiume ndiye mrembo zaidi, mbali na jamii ya binadamu. Naye mwanamume ana sura mbaya, na mwanamke ni mrembo. Hiyo ni kweli. Ukimwona mwanamume ambaye ni maskini kitu cha kupendeza, kumbuka tu, kuna seli mahali iliyowekwa mahali pasipo pake mahali fulani.

96 Sasa, hilo linapaswa kutufanya sisi sote wenye sura mbaya tujisikie vizuri. Lakini ni, unapomwona mwanamume akionekana na kutenda kama mwanamke, kuna upotovu mdogo sana pale mahali fulani. Kisha ukimwona mwanamke akijaribu kutenda na kuonekana kama mwanamume, imepotoshwa hapo tena. Wote wawili walikuwa wa kiume mwanzoni, ndipo Mungu akawatenganisha, Akaweka roho ya kiume ndani ya mwanamume, na kuchukua roho ya kike, na kuiweka ndani ya mwanamke. Basi unapomwona mwanamume akijaribu kuwa wa kike, ama—ama mwanamke akijaribu kuwa mwanamume, kuna kasoro mahali fulani.

97 Angalieni, kusudi wapate kuwa mmoja, nafsi na mwili pia, Yeye alitoa ubavu ubavuni mwake, na kumfanya mwanamke. Mnaona? Mwanamke hayuko katika uumbaji wa asili, yeye ni zaotuka la mwanamume. Mnaona? Leo hii katika Marekani yeye ni bosi, kijimungu, na chochote kile. Atashuka akijinyonga-nyonga mtaani na kuwapeleka watu wengi zaidi kuzimuni kuliko vilabu vyote vya pombe haramu mnavyoweza kuweka kati ya hapa na Los Angeles. Hiyo ni kweli.

98 Lakini hata hivyo, mwanamke mzuri ndicho kitu kizuri sana ambacho Mungu angeweza kumpa mwanamume, kwa sababu ni sehemu yake. Lakini kuhusu hii Hollywood hapa chini, na mashimo kama hayo ya kuzimu, yameliharibu taifa na maisha ya taifa, na kuuvunja uti wa mgongo kupitia utovu wa uadilifu wa wanawake na umama, kupitia mahakama za talaka na kadhalika.

Ni—nitaliondokea somo langu. Nitalirudia tena wakati mwingine.

99 Inavutia. Sasa, anaifanya tena, anaifanya ya kielimu, ya kiakili. Hivi Roho Mtakatifu hakutwambia katika Timotheo wa Pili, mlango wa 3, kwamba katika siku za mwisho lingekuwa ni kundi la wasomi kanisani? "Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasingiziaji, wasiojizuia, na wasiopenda hao walio wema."

Unasema, "Hao ni wakomunisti."

100 Loo, la, hao ni wanaojiita Wakristo. Mnaona? "Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake." Nazo hizo nguvu ni Neno lililodhihirishwa. Kasema, "Injili ilitujia si kwa Neno tu, bali kwa nguvu na madhihirisho ya Roho." Ninazungumza juu ya jeshi la Mungu sasa, lililoimarishwa.

101 Huifanya ya kuvutia, tajiri, inayometameta. Loo, kila kitu kinametameta kwa Hollywood, shimo la biashara haramu la

dunia. Na ilikuwa kwamba tulienda Paris kupata mitindo ya wanawake wetu, na sasa Paris huja hapa kuichukua kutoka kwetu. Nilihubiri, hapa siku moja, juu ya *Uvamizi Wa Marekani,* na *Kupinduliwa Kwa Serikali Ya Marekani*, mnapaswa kuusikiliza. Nilikuwa na maskini kiruka njia aliyeketi jukwaani, ama, maskini mnenguaji, anavyoitwa, na kusema, "Huyu *hapa*." Na—na hiyo ni kweli.

102 Lililo duni sana kwa mataifa yote, talaka nyingi zaidi Marekani kuliko zilizoko ulimwenguni kote zikiwekwa pamoja, karibu hivyo. Ustaarabu mpotovu, mchafu, wenye kinyaa, na wa mwisho, nasi tuko kwenye Pwani ya Magharibi, ambako mashariki na magharibi zitakutana. Hiyo ni kweli. Moja kwa moja katika makanisa yetu wenyewe, moja kwa moja miongoni mwa watu wetu wenyewe.

103 Lakini Shetani hulifanya la kuvutia. Bila shaka, linavutia, dhambi inavutia. Lakini adui anaendelea kupata chambo bora zaidi. Yeye atamvua nguo zaidi kidogo, na kufanya *hivi*, na kufanya *vile*. Wala msijali, kamwe hatamfanya uchi kabisa, angekuwa na sura mbaya sana wakati huo. Mnaona, yeye kabisa anajua la kufanya. Lakini Shetani anaendelea kuingiza dhambi, na hiyo ilikuwa ndiyo ile dhambi ya asili. Hapo ndipo anapotokea, kwa kitu kile kile kama ufalme ulivyokuja, vita.

104 Sasa, angalieni, bali haimlazimu Mungu kufanya jambo lolote la zaidi kwa walio Wake, kulifanya livutie zaidi. Jambo pekee analopaswa kufanya ni kuinua tu kiwango cha Neno Lake Mwenyewe dhidi ya adui. "Wakati ninii . . ." Biblia ilisema, "Adui anapokuja kama mafuriko, Roho wa Mungu huinua kiwango dhidi yake." Yeye hufanya nini? Yeye hulifanya Neno, ambalo tayari amelinena, kuwa la hakika zaidi. Whiu! Kuchukua Neno Lake lile lile, na kulifanya halisi zaidi.

105 Sina pochi yangu, lakini hivi ulipata kuona nyuma ya dola ya Marekani? Upande mmoja ina muhuri wa Marekani, tai mwenye mishale kwenye kucha zake, muhuri wa Marekani. Lakini kwenye kona nyingine inayokukabili, naamini kona ya upande wa kulia, ina piramidi, naye ameandika hapo chini, "Muhuri Mkuu."

106 Kwa nini taifa letu liwazie kuifanya, piramidi ya Misri, "Muhuri Mkuu," hata kuuzidi muhuri wetu wa tai wa Marekani? Hivi mliona juu tu ya piramidi kuna jiwe la kichwa limesimama juu yake, kama jicho linaloangaza?

107 Sasa, nimekuwa Misri, na katika hizo piramidi, jinsi ningeweza kuchukua alasiri yote! Sasa, siamini katika mafundisho ya piramidi, ninatoa tu mfano. Lakini unapoona hiyo piramidi, kamwe haikupokea hilo jiwe. Henoko aliijenga, piramidi hi—hiyo, katika siku zake. Hawawezi kuelewa.

108 Sasa, wana kila namna ya dini juu yake, kama walivyo nazo katika zodiaka. Lakini kila kitu katika . . . Mungu aliandika

Biblia tatu, ya kwanza ilikuwa mbinguni, ya pili ilikuwa katika piramidi, ya tatu iko duniani, na kila moja inakubaliana na hiyo nyingine.

109 Angalieni, zodiaka inaanza na kitu gani? Bikira. Inaishia na nini? Leo yule simba; kule Kuja mara ya kwanza kwa Kristo, na Kuja mara ya pili kwa Kristo. Nasi sasa tuko katika samaki waliokingamana, ambao ni wakati wa kansa, kikamilifu. Angalieni huu—huu mnara hapa, pi—piramidi, mwanzoni ni pana sana, inayofuata inaelekea kwenye uchache, kisha inakaribia tena, ndipo lile Jiwe la kichwa linakuja.

110 Ilikuwa ni kitu gani? Luther katika yale matengenezo, kuhesabiwa haki, ndipo adui akaanza kuja kama mafuriko, akainua kiwango, utakaso, wenye nguvu zaidi katika Roho. Ndipo wakati adui alipoanza kufunika hilo nao wakaanza kujiundia dhehebu na kujiunga na *hiki*, *kile*, na *kinginecho*, ndipo Roho wa Mungu akaingia ndani ya Wapentekoste, ubatizo wa Roho Mtakatifu, wakaunda madhehebu na kuondoka. Sasa, Yeye anafanya nini? Hakuna wakati mwingine utakaokuja, bali Yeye analichukua kanisa hilo la Kipentekoste na kuwaondoa Wateule kutoka kwake, na kulichonga ili kwamba wakati Jiwe hili la kichwa litakapokuja juu Yake, itabidi liwe kama hayo mengine.

111 Mbona, ni kwamba, hayo mawe yaliyowekwa kule juu yakiwa na mamia ya tani, yamewekwa kule juu yameumana sana bila saruji hata huwezi kupitisha wembe kati yao. Ndipo basi wakati lile Jiwe la Kichwa litakapokuja, Kristo atakapokuja kwenye Hekalu Lake, italibidi liumane kikamilifu kama mengine yote. Nayo huduma ya kanisa la Kipentekoste itabidi iwe kamilifu sana mpaka itaingiana moja kwa moja na huduma ile ile aliyokuwa nayo hapa, ambapo litachukua Kitu hicho chote katika Unyakuo, likiwa ni Kanisa. Hiyo ni kweli.

112 Sasa, "Adui anapokuja kama mafuriko, Yeye huinua kiwango dhidi yake." Sasa angalia, katika Edeni Yeye aliwapa Neno Lake kama Silaha zao, Neno tu lililonenwa. Ndipo adui akaja kama mafuriko, Naye akalichukua Neno na kulifanya mwili likae miongoni mwetu, lenye nguvu zaidi kidogo. Kutoka Huko juu akizungumza, Huyu hapa akitembea duniani. Utukufu! Mtaniita "mtakatifu anayejibingirisha" kwa vyovyote vile, kwa hiyo afadhali mlizoee sasa.

113 Loo, kwanza lilikuwa ni Neno Lililonenwa huko nje, sasa Hili hapa, ungeweza kuligusa, lilifanyika mwili. Ndipo basi wakati adui angali anaingia kama mafuriko, alilimwaga Neno ndani ya mtu huyo, akiwa umbo la Roho Mtakatifu. Hizo hapo *moja*, *mbili*, *tatu* zako tena, kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kama vile Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, na kadhalika, katika ukamilifu.

114 Sasa, angalieni Neno Lililonenwa. Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu; Neno juu yetu, Neno pamoja nasi, Neno ndani yetu. Haleluya! "Ninyi ni wa Mungu," jeshi la Mungu, likisonga mbele. Neno la Mungu lililonenwa juu yetu katika Nguzo ya Moto, Dhihirisho la Mungu la Neno Lake katika mwili, sasa Roho wa Mungu, Neno Lililonenwa, ndani yetu. Amina. Loo!

115 Sasa, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, kulikuwako na majitu nchini, mwajua. Na kwa hiyo, Shetani pia ana mabingwa wake wa kielimu nchini. Hiyo ni kweli. Loo, jamani, D.D., D.D., Ph., L maradufu. Loo, jamani, jamani, jamani! Mabingwa wa kielimu. Loo, wanajua maneno yote, sarufi yote, wanajua, wanajua tu yote, mabingwa wa kielimu, lakini *kwa njia moja ama nyingine* wanakuwa majasusi, na huo ni mfumo wa kijasusi. Samahani sasa, ndugu msomi, lakini ni mfumo wa kijasusi unaoingia kisiri miongoni mwenu kuwachukua kondoo na kusema, "Mbona, ha—hao ni watakatifu wanaojibingirisha! Sivyo ilivyo." Kama inaambatana na Neno, *ndivyo* ilivyo.

116 Sasa, tunajua tuna vitu bandia kila mahali. Hiyo ni kweli. Ni vita, huna budi kumjua adui wako, nawe huna budi kujua Silaha zako, Silaha zako ni Neno. Adui wako ni kitu kitakachohoji dhidi Yake. "Sasa, nakwambia, mpenzi, si lazima ufanye *hivi*. Kanisa letu ndilo kanisa kubwa kuliko yote. Tuna zaidi . . ." Huh, uh-huh. Bingwa wa kielimu, nawe ukimsikiliza kwa dakika chache, atakupeleka mbali sana na ile Kweli, hata hutajua mahali ulipo. Hiyo ni kweli. Loo, mdanganyifu sana, ukosi wake umepinduliwa, mwajua, naye anashuka chini, na kusema, "Vema, tunaninii . . . Tumekuwa safarini kwa muda mrefu, mrefu sana."

117 Mwajua, hapa si muda mrefu uliopita niliona ambapo pa—papa wa Rumi aliyaalika makanisa yote yarudi kwenye mwanzo. Nikasema, "Mungu asifiwe, ningetaka kufanya hivyo."

118 "Ninyi nyote rudini Rumi, ambapo Kanisa lilianzia." Ningependa mwanahistoria fulani, msomaji fulani wa Biblia, ama mwanachuoni fulani anithibitishie ya kwamba Kanisa lilianzia Rumi. Kanisa lilianzia Yerusalemu kwenye Siku ya Pentekoste, hapo ndipo Kanisa lilipoanzia. Rumi haikuwa na uhusiano wowote nalo. Rumi ilikuwa ndiyo maangamizi Yake wakati ilipounda madhehebu.

119 Lakini nitawaambia madhehebu yalianzia Rumi. Hiyo ni kweli. Lakini Kanisa katika kuzaliwa Kwake, katika Silaha Zake, lilianza kwenye Siku ya Pentekoste huko Yerusalemu. Basi endapo mheshimiwa papa anataka kurudi kwenye wakati huo, nitaungana naye, na kusema, "Mungu atukuzwe, nitaweka kila kitu niwezacho kwa ajili yako." Ninajaribu kurudi kwenye Siku hiyo.

120 Ujumbe wa siku za mwisho, yule mjumbe wa Nuru ya jioni, kulingana na Malaki 4, atakuwa akiigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ule Ujumbe wa asili, wa Kipentekoste. Umevurugwa sana, na kadhalika, huku nje. Lichukue Neno la Mungu.

121 Wapelelezi wako nchini. Loo, jamani! Wanapenda kubishana nawe. Mtu alinijia hapa si muda mrefu uliopita, naye alishikilia, kwamba, "Ni wale mia na ishirini tu waliopanda ghorofani, ni wale mitume kumi na wawili pekee waliompokea Roho Mtakatifu, uponyaji wa Kiungu. Tunanena mahali Neno linaponena, tunanyamaza mahali limenyamaza," na kuendelea namna hiyo. Nilimwacha tu apayuke kwa muda kidogo, kama bundi wa Kiairishi, mipayuko mitupu na manyoya wala hamna bundi kwa vyovyote vile. Kwa hiyo akamalizia hivyo.

Nikasema, "Ngoja, unapaswa kunipa nafasi kuelezea jambo hilo. Je, ulisema kulikuwa na mitume kumi na wawili pekee waliompokea Roho Mtakatifu?"

"Naam."

122 Nikasema, "Basi Paulo hakumpokea. Ati karama ya uponyaji ilipewa wale kumi na wawili pekee, ulisema? Basi vipi kuhusu Stefano, aliyeshuka akaenda na kuwahubiria Wasamaria, na kuwawekea mikono, na kutoa pepo katika ule uamsho mkuu? Vipi kuhusu Paulo akishuka na kuweka mkono wake, uh, Petro akashuka akaja, akaweka mikono yake juu yao nao wote wakampokea Roho Mtakatifu? Vipi kuhusu Matendo 10:49 wakati Mataifa walipopokea ule wito? Mshangao wa *tohara*, juu ya Mataifa pia kilimwagwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa waliwasikia wakinena kwa lugha na kumtukuza Mungu. Ndipo wakasema, 'Je, tunaweza kukataza maji, kwa kuwa hawa hawapaswi kubatizwa ambao wamempokea Roho Mtakatifu kama tulivyompokea hapo mwanzo?'" Amina. Utukufu! Hiyo ni kweli.

123 Loo, nina furaha sana kuweka matanga kwenye pepo za Upepo wa nguvu ukienda kasi, nawe je? Zinakupitisha moja kwa moja katika Biblia, Andiko kwa Andiko.

124 Lakini ili kuharakisha, mabingwa hawa wa kielimu wamezidi sana kwa watu wanyenyekevu wa Mungu. Sasa, watu wa Mungu daima wamekuwa wasio na elimu na wanyenyekevu. Niambieni tu wakati mmoja ilipokuwa vinginevyo. Waangalie wale wana wawili, waangalie watoto wa Kaini na Sethi. Habili aliuawa, ambalo lilikuwa ni mfano wa mauti, kuzikwa, na kufufuka kwake Kristo, Sethi akachukua mahali pake.

125 Sasa, watoto wa Kaini wakawa wasomi, wa kidini, maana baba yao alikuwa ni mtu wa kiakili, Kaini, wa kidini. Naye Kaini akajenga madhabahu, Habili akajenga madhabahu; Kaini alitoa dhabihu, Habili akatoa dhabihu; Kaini aliabudu, Habili akaabudu. Na kama Mungu analiheshimu tu kanisa, utaratibu

wake, ibada zake, matoleo yake, na kadhalika, kama hayo ndiyo yote Mungu anayoheshimu, hakuwa na haki kumhukumu Kaini, maana alikuwa tu wa kidini kama Habili alivyokuwa, bali hakuja kwa njia sahihi.

126 Vipi kuhusu Moabu? Kulikuwako na Israeli, kulikuwako na Moabu, waliomwabudu Mungu yeye yule tunayemwabudu. Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni mtoto wa binti ya Lutu. Nao hao hapo, walitoka wakamleta Askofu Balaamu, naye akajenga madhabahu saba, kama tu walivyokuwa huko Israeli.

127 Sasa, Israeli hawakuwa wa kimadhehebu, hawakuwa na taifa la kuliendea, bali walikuwa wakiendea moja. Amina. "Hapa hatuna mji udumuo, bali twautafuta Ule ujao." Angalieni, Balaamu alitoa dhabihu saba safi, mafahali, kama tu walivyofanya huko Israeli, naye Balaamu akatoa kondoo dume saba, akinena juu ya Kuja kwa Kristo, vivyo hivyo na Israeli.

128 Basi mambo ya kimsingi ndiyo Mungu anayohitaji, sehemu zote mbili zilihesabiwa haki. Lakini ilikuwa ni kitu gani? Ni kitu gani ambacho Balaamu alishindwa kuona? Alishindwa kuiona Nguzo ile ya Moto, alishindwa kuona ule mwamba uliopigwa, ile nyoka ya shaba iliyowatangulia Israeli kwa ajili ya upatanisho, alishindwa kusikia yale makelele ya kambi, ya Mfalme miongoni mwao. Aliwahukumu kwa matendo yao; Mungu hamhukumu mtu yeyote kwa matendo yao, anakuhukumu kwa imani yako.

129 Angalia, ninataka kufafanua jambo hilo, kuhusu maskini yule mwanamke jana usiku, pia. Haikuwa ni kazi zake za kuosha ninii yake. . .miguu. Yeye alimhesabia haki wakati huo mbele ya Simoni kwa kusema yale aliyokuwa amefanya, Yeye alimhesabia haki kwa matendo, yale aliyokuwa akifanya. Lakini alipomhesabia haki machoni pake mwenyewe, Yeye alisema, "Imani yako imekuokoa," maana hakuna mtu ahesabiwaye haki kwa matendo. Kwa imani yake katika Yeye kuwa ni Mwana wa Mungu, si yale aliyokuwa akifanya, bali imani yake Kwake. Nayo imani yako daima huonyesha matendo yako. Hiyo ni kweli.

130 Hawa mabingwa wa kielimu walikuwa, katika siku hizo walikuwa mbali. . .wao. . .Angalieni kile watoto wa Kaini walichofanyika: wanasayansi, madaktari, wafua chuma, watu mashuhuri duniani. Lakini watoto wa Sethi walikuwa nini? Wakulima, wachunga kondoo. Mnaona? Hawangeweza kujilinganisha nao hata kidogo, naye Mungu alitufananisha na kondoo.

131 Kama mtu yeyote alipata kufuga kondoo, kondoo ni, kitu kimoja, akipotea, amepotea kabisa. Hawezi kwenda popote bila mchungaji. Na hivyo ndivyo Mungu alivyotuumba, hatudai kuwa na akili, tunaye Mchungaji tu, hivyo tu, Naye anatupeleka kutoka malisho hadi malisho.

132 Kwa hiyo siku hizi majasusi hawa wakuu wa kielimu wamewazidi sana maskini watoto wa Mungu wanyenyekevu.

Sasa, Yuda alisema, katika Kitabu cha Yuda, mwisho wa . . . Yuda pale, alisema ya kwamba, "Wamejiingiza kwa siri miongoni mwetu," wamejiingiza kwa siri. Mnaona? Hilo ndilo linalosababisha kutoka katika hamaki hizi kubwa ambazo wamefanya. "Walijiingiza kwa siri miongoni mwetu, watu walioandikiwa hukumu hii tangu zamani."

133 Wamejiingiza kisiri miongoni mwetu, wakituondoa kwenye Neno, wakitufanya tupoteze imani katika Neno, imani zinazotangatanga, meli zisizo na mwelekeo. Upepo unaoenda kasi ungeweza kuvuma, nao wana nguzo tu ya dhehebu la kale iliyokufa imesimama pale, ikifanya, "*Wuuuh!* Siku za miujiza zimepita. *Wuuuh!* Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu."

134 Lakini kama una tanga halisi la kiroho lililowekwa kule juu, Roho analichukua naye huyo anaondoka anaenda kwenye nchi ambazo hawajui lolote kuzihusu. Kweli. Naam.

135 Wakikufanya upoteze imani katika Neno kwa ujuzi wao wa seminari uliopigwa msasa. Walimshambulia Nuhu vivyo hivyo, wamewashambulia watoto wa Mungu kila wakati vivyo hivyo. Nimrodi alijijengea mnara apate kuyaepuka mapigo ya Mungu, bali haukudumu, Nebkadreza alijijengea mji, lakini ukaanguka.

136 Nuhu, akijenga safina, ungeweza kuwazia wanasayansi katika siku hizo ambao wangeweza kujenga piramidi ambayo tusingeweza kujenga siku hizi, wangeweza kuhifadhi mwili kwa ugiligili tusiojua chochote juu yake? Mambo mengi ambayo hatujajifunza bado ambayo wao waliyajua. Ungeweza kuwazia hao wanasayansi wakisema, "Ewe maskini tapeli! Nionyeshe. Tunaweza kurusha rada yetu kwenye mwezi na kadhalika, hakuna hata tone la maji kati ya hapa na kule. Itakujaje?"

137 Lakini Nuhu alisema, "Mungu, kama Yeye aliahidi maji, anaweza kuweka maji huko." Mnaona? Hakika. Imewazidi sana watoto hawa siku hizi, maskini watoto hawa wadogo, wenye elimu.

138 Loo, angalieni ile siku ya . . . wakati Yehoshafati aliposhuka na kuondoka mahali pake, naye akakutana na Ahabu. Naye Ahabu, sikuzote ana sababu zake, basi akasema, "Je, Ramoth-gileadi si mali yetu?"

Kasema, "Hakika, Yoshua, katika kuigawa nchi, alitupa sisi."

Kasema, "Vema."

139 Lakini mnajua, Yehoshafati alikuwa ni mtu mzuri, lakini nje tu ya mahali pake. Hiyo ndiyo shida ya watu wengi siku hizi katika baadhi ya nyumba hizi za maiti za kiroho, michirizi ya barafu imening'inia humu ndani, kipimajoto, tukinena kiroho, kwenye tisini chini ya sufuri. Ukiingia mle, na kusema, "Amina," ama "Mungu asifiwe," kila mtu ananyoosha shingo yao kama bata bukini fulani, na kuangalia kote, kuona kilichotukia.

Wamekufa, wamekufa mara mbili, wakang'olewa pamoja na mizizi. Wanasahau kuhusu . . .

140 Nilikuwa nikihubiri usiku mmoja, ndipo mwanamke mmoja akaanza kupiga mayowe na kupaza sauti, maskini ndugu mmoja Mbaptisti akaniambia, kesho yake akasema, "Nilikuwa nikifurahia ujumbe wako mpaka mwanamke huyo alipoanza kupiga mayowe." Kasema, "Unajua hilo lilifanya baridi kupitia mgongoni mwangu."

141 Nikasema, "Ndugu, unaishi katika ulimwengu mtulivu kuliko wote uliowahi kuishi. Ukienda kuzimuni, kutakuwako na kulia na kuomboleza na kusaga meno. Ukienda Mbinguni kutakuwa na kupiga mayowe na kupaza sauti wakati wote. Mbona," nikasema, "Jamani, kama hiyo ilifanya baridi iingie mgongoni mwako," Nikasema, "itafanya nini utakapofika Mbinguni? Mbona, utaganda hata kufa utakapofika Kule!" Nikasema, "Ungekuwa mahali si pako. Kwa kuwa hata Malaika, wakiwa na mabawa juu ya uso wao na mikono, uh, juu ya miguu yao na juu ya miguu yao na juu ya uso wao, wanaimba, 'Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu!'"

Mungu ni kitu cha kuabudiwa, Mungu ni kuabudiwa, kuabudiwa. Kama ninawaheshimu Wapentekoste kwa jambo lolote, ni kujiachilia na kumwabudu Mungu. Naam.

142 Mabingwa wa kielimu. Hapo alisimama Yehoshafati, aliyezoea kumwabudu Mungu, huyu hapa alikuwa Ahabu. Naye Yehoshafati, bila shaka, akiwa ni mtu wa Mungu, alifikiri jambo la kwanza ni kumtaka Mungu shauri. Hilo ndilo jambo bora zaidi. Yeye alisema, "Inatupasa kumtaka shauri Mungu."

143 "Loo," Ahabu akasema, "hakika, Mheshimiwa, Bwana, Mfalme wangu. Naam, Bwana, Mheshimiwa. Mbona, hakika! Nina seminari moja hapa chini iliyojaa hao, nina mia nne wa walio bora kuliko wote waliopo."

Kasema, "Hebu waite."

144 Na hapa akaja Daktari, Ph.D., L.L, wote wakaja kule, naye Mikaya akaja, na hao wote wakaja kule, uh, si Mikaya. Manabii wote wakaja kule, nao wakasema, "Tabiri na utwambie: Je, twende Ramoth-gileadi, ambako Yoshua, Mungu alitupa nchi hiyo?"

Nao wakashuka wakaenda, na kumtaka Mungu shauri, nao wakaomba, na kuomba, wakarudi na kusema, "Naam, kwea, Bwana yu pamoja nawe."

145 Hezekia akaenda na kujitengenezea pembe kubwa mno, akapitia mbio kwenye umati, kasema, "Kwa hizi, pembe hizi kubwa za chuma, utaisukuma Ramoth-gileadi . . . utawasukuma Wafilisti moja kwa moja nje ya nchi, ama, Washami. Utawasukuma moja kwa moja nje ya nchi kwa hizi."

"Loo! Sasa, hebu na tutoe hoja. Sasa," kasema, "unajuaje kwamba ndivyo ilivyo?"

"Angalia hapa, Mungu alitupatia nchi hiyo. Chakula kinacholimwa kwenye nchi hiyo kinawaendea Israeli, Mungu alitupa sisi kupitia Yoshua."

"Amina," wote wakasema. "Hiyo ni kweli, Bwana, Mheshimiwa."

"Naye adui yetu anajinenepesha katika nchi yetu, si vizuri."

"Amina. Hilo linasikika la kupendeza."

146 Si linasikika la kupendeza, kiakili? Lakini unajua, kuna kitu kama hicho, ambacho mara nyingi hakimgusi mtu wa Mungu. Yehoshafati akaangalia kote, akasema, "Hawa tu ndio wote ulio nao?"

147 "Mbona," akasema, "tuna mia nne hapa wenye moyo mmoja! Mbona, shule nzima iko hapa nje! Seminari zote ziko pamoja, zote ziko hapa."

148 Kamwe kwa namna fulani halikukolea; huyo alikuwa ni yule Uzao aliyechaguliwa tangu zamani, mnaona, hapa.

Akasema, "Hivi huna mmoja tu zaidi?"

149 Kasema, "Naam, nina mmoja zaidi, lakini ninamchukia. Namchukia." Kasema, "Ni Mikaya, mwana wa Imla." Lakini kasema, "Ninamchukia, kwa sababu sikuzote ananitabiria mabaya." Loo, ndugu! Mungu ambariki mtu huyo. Akasema, "Hapa kuna kila moja ya madhehebu yetu, kila mmoja wao katika moyo mmoja," kama vile U.N. huko juu sasa.

150 Mnajua Biblia ilisema Yeye ange—Yeye angekusanya magugu kwanza. Hakika yanaungana pamoja, yote kwa Baraza la Makanisa Ulimwenguni, kila moja lao likienda, huko ndiko yote yanakoelekea. Hilo linalipa Kanisa nafasi ya kukua basi. Vema. Wana mateso madogo ambapo hawalishwi vizuri sana na kila kitu, inabidi wasukumwe pamoja. Mungu ana njia ya kufanya mambo, mwajua.

Kwa hiyo muda si muda mwajua, kwamba wote... Yeye alisema, "Tuma mtu akaletwe. Hebu na tumsikie, tuone atakachosema."

Akasema, "Ninakuonya kabla hajaja, jamaa huyo hafanyi chochote ila kunipayukia wakati wote."

"Loo, mfalme asiseme hivyo."

151 Kwa hiyo wakatuma halmashauri ya mashemasi huko kumleta, wakafanye mkutano huu. Kwa hiyo walipopata... walipokuja wakampata, walisema, "Angalia, Mikaya, unajua nini? Umefukuzwa kwenye shirika, unaelewa. Wewe huko katika ushirika tena, ilitubidi kukufukuza. Nami nakwambia sasa, unajua, nawe ni Mwisraeli, kama tulivyo sisi, unajua ya kwamba Ramoth-gileadi ni mali yetu.

152 "Sasa, nitakwambia la kufanya, kama unataka kupata kibali, na kurudi katika nafasi yako nzuri tena pamoja na—pamoja na hao ndugu, nakwambia utakalofanya, nenda kule na kusema jambo lile lile wanalosema."

153 Ndugu, alikuwa amekosa shabaha wakati huo. Upuuzi wa namna hiyo hauendani na mtu wa Mungu, nabii. Alijua kilichomwimarisha ni Neno la Mungu.

Akasema, "Kama Bwana aishivyo, nitasema tu yale atakayoweka kinywani mwangu." Loo, amina. Haya basi. Sema tu . . .

154 Sasa, kama yeye . . . Mtu fulani akisema, "Hivyo ndivyo ninavyofanya, pia." Kila mtu angejaribu kusema hivyo, lakini kama akiweka kitu mle ndani kinyume cha Neno Lake, ilikuwa ni ibilisi aliyekiweka mle ndani, sio Mungu. Mungu huliweka tu Neno Lake.

155 Angalia mahali nabii huyo anapoelekea, Yeye alijua Neno la Mungu liliwajia manabii. Naye Eliya, nabii, tayari alikuwa amemlaani Ahabu kwa sababu ya Nabothi, na kusema ya kwamba mbwa watairamba damu yake. Kwa hiyo Mungu angewezaje kubariki kile alichokuwa amelaani?

156 Kwa hiyo Mikaya akasema, "Ngojeni, nami nitaona atakayosema." Angalieni atapata ono kwanza na kulilinganisha na Neno. Hiyo ni sikuzote. Lilinganishe na Neno, hilo ndilo Urimu na Thumimu ya Mungu. Kwa hiyo basi, a—alipoenda, kasema, "Nipeni usiku huu." Basi usiku huo, huenda aliomba usiku kucha, ndipo Bwana akamjia, akamwambia la kusema.

157 Akashuka, kesho yake asubuhi, akasema, "Kwea, hiyo ni kweli, bali nimewaona Israeli wametawanyika kama kondoo, bila mchungaji."

158 Mnaona? Alikuwa amefanya nini? Alikuwa tayari amelinganisha ono lake na Neno, naye alijua alikuwa kikamilifu kabisa, pale. Haidhuru ni wasomi wangapi mashuhuri, wakubwa, waliofunzwa shuleni, na wanachuoni walioadibishwa, na seminari, hilo ha—halikumsumbua Mikaya hata kidogo. Kwa nini? Alidumu ameimarishwa na ono lake la Neno. Huyo hapo.

159 Mmoja wao akampiga kofi mdomoni, kasema, "Sasa, kamwe hatutakuingiza kwenye shirika." Kasema, "Hebu nikuonyeshe jambo fulani, Mikaya. Je, si ni jambo la busara . . .?"

160 Sijali ni "la busara" jinsi gani, kama ni kinyume na Neno la Mungu, ni kinyume na Neno la Mungu. Kama jitu la kielimu likija, kasema, "Hatumhitaji Roho Mtakatifu yeyote. Hatuuhitaji uponyaji huu wa Kiungu." Hilo, sijali linaonekana la busara jinsi gani, kama ni kinyume na Neno, Mungu alitoa ahadi. Amina.

161 Wanasema, “Hiyo ilikuwa tu kwa ajili ya mitume.” Nashangaa tu wanapata wapi. . .Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, “Tubuni, kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Amina. Ati kwa ajili ya mitume tu? Ni kwa kila mtu aliyeitwa. Naam, usilisikilize jitu hilo. Unaona?

162 Tunashindana, Biblia inasema hapa, si juu ya damu na nyama. Hatujaribu kuvunja mashiko ya vidole katika uwanja wa miereka kwa nyama na damu, bali tunajaribu kuvunja mashiko ya moyo ya pepo waliowashika watu, wakaingia kwenye mfumo wao, ndani ya moyo wao, kuwafanya wafanye na kusema mambo yasiyofaa. Hakika.

163 Nilikuwa nikininii. . .Mwajua, mimi mwenyewe ni mwanandondi wa zamani. Nilipata. . .nilikuwa na Ubingwa wa uzito wa Bantamu usioshindwa wa majimbo matatu—matatu. Nilikuwa nikiwaangalia hao jamaa wakija kwenye ulingo na madoido ya kila namna, wamejitundika madoido yote. Hilo halikuwafanya wapiganaji, wakati mwingine hilo lilikuwa ni uigizaji. Hilo halikukuhusu wewe. Kama hukuwa na nguvu zilizofichwa pale za kuvunja hayo mashiko!

164 Na hivyo ndivyo tunavyojaribu kuyaleta makanisa yetu siku hizi, yakiwa na mnara ulio juu sana, viti vya kupendeza kuliko vyote, umati uliovalia nadhifu zaidi. Hilo halivunji mashiko ya vidole. La, inahitaji nguvu hizo zilizofichwa za Roho wa Mungu, Neno hilo mle ndani kuvunja hayo mashiko. Hiyo ni kweli.

165 Kama vile Petro alivyokuwa, alikuwa hodari kwa upanga wake. Yesu alipoingia katika shida, aliuchomoa upanga wake, angeweza kushambulia kwa njia yoyote, na kumkata kuhani mkuu, sikio la mtumishi wake kwa upanga, lakini ilipofikia kwenye ujasiri halisi wa Kikristo, hakuwa nao. Naam. Lakini ule ujasiri wa kiroho, yeye alikana Neno lililofanyika mwili likisimama moja kwa moja miongoni mwao.

166 Alikuwa hodari kwa upanga wake, hiyo ni kweli. Angeweza kupigana na kanuni ya imani vizuri tu kadiri mtu yeyote alivyoweza, lakini yeye, ilipofikia kwenye ujasiri wa kiroho, hakuwa nao. Kwa hiyo akashindwa papo hapo. Sasa, kwa nini? Alijua tu jambo moja, kanuni yake ya imani. Lakini ndugu, baada ya kwenda Pentekoste, alivaa Silaha zote za Mungu. Sasa, mwangalieni, yeye ni mtu tofauti sasa, alivaa Silaha zote.

167 Ilikuwa ni kitu gani? Neno hilo alilokuwa ametembea nalo lilikuwa ndani yake, likimchoma kwa Moto mwilini na nafsini mwake, alikuwa amevaa Silaha zote za Mungu. Hiyo ni Silaha iliyotolewa na Mungu. Alikuwa na ubatizo, amejazwa na Roho Mtakatifu. Ni kitu gani? Mungu hujifanya kuwepo daima katika

jeshi Lake Mwenyewe. Mungu, kwenye Siku ya Pentekoste, alishusha Silaha zote za Mungu kwa ajili ya jeshi Lake, ambayo ilikuwa ni Yeye Mwenyewe miongoni mwenu.

168 "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona, kwa sababu nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Mathayo 28. Vema. Kwamba Yeye ana . . . Yeye yuko pamoja nasi, ndani yetu, Hiyo ndiyo Silaha, ni Yeye. Yeye ni Neno, Naye ni Roho Mtakatifu, naye Roho Mtakatifu yuko ndani yetu, ambaye ni Neno likiidhihirisha ile ahadi. Hii ndiyo ahadi, Kristo ni Neno, Naye hulidhihirisha.

169 Roho hulihuisha Neno, hufanya ninii . . . Kwa maneno mengine, Yeye ndiye Baruti inayorusha risasi kutoka pale pamoja nalo. Kama ilivyokuwa ni Baruti wakati Daudi alipokutana na Goliathi akiwa na kombeo lenye jiwe ndani yake. Alikuwa na mahali pamoja tu pa kupiga, na hapo palikuwa papo *hapo* katikati, kwingine kwote kulikuwa na silaha, bali Mungu akaingia katika roho hiyo.

170 Ilikuwa ni kitu gani? Alikuwa na mawe matano na kombeo. Angalieni, i-m-a-n-i *katika* Y-e-s-u [Kiingereza: J-e-s-u-s—Mfa]. Huyu hapa anakuja, jambo fulani liko karibu kutukia, maana hilo hapo Neno, ile ahadi, na nguvu za kulirusha kwa kombeo. Hilo ndilo tunalohitaji siku hizi, ni mtu atakayelichukua Neno la Mungu pamoja na nguvu za Roho Mtakatifu nyuma yake kulisukuma huko nje na kuliangalia likitimia. Hilo ni jeshi la Mungu. Amina. Neno Lake la Moto, jeshi Lake lote limevaa Uwepo Wake udumuo mle ndani, akienda pamoja nasi. "Nitaenda pamoja nanyi, niwe ndani yenu. Si wewe unenaye, Baba anayekaa ndani yako, Yeye huzitenda hizo kazi."

171 Katika jeshi Lake, Yeye huwasilisha jeshi Lake katika mfano wa ofisi tano, kwanza, mitume, manabii, waalimu, wachungaji, wainjilisti. Hilo ndilo jeshi Lake, hao ndio askari Wake, hao ni wakuu Wake wa vikosi, wote wakiwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, wakingojea huko nje kukutana na adui kwenye viwanja vyovyote atakavyojia, kukutana na adui kwa Neno la Mungu. Amina. Kila mmoja akiungana na mwenziwe, pamoja Naye, Kapteni Mkuu, si huko nje mbele, *hapa* juu, huko nyuma, bali *ndani* yao. Amina. Hilo ndilo jeshi. Likithibitisha. Kuthibitisha nini? Kufufuka Kwake, kwa thibitisho la kazi Zake.

172 Yohana 14:12, Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Ni kitu gani? Ni Mungu Kanisani katika ofisi hizi tano zilizochaguliwa tangu zamani, akiunga mkono kila Neno alilosema akiwa na Roho Mtakatifu Mwenyewe mle ndani, ambaye ni Neno lililodhihirishwa, akithibitisha kufufuka Kwake, akithibitisha ya kwamba Yeye yu hai.

173 Dini zingine zote zimekufa, taratibu zao zimekufa, kuna moja tu iliyo ya kweli, na hiyo ni Ukristo, kwa sababu Kristo anaishi katika Kanisa la Kristo, amina, akiyadhihirisha Maneno Yake, kwa kuwa Yeye ni yule yule. Kama ni Neno lile lile, litafanya mambo yale yale, na kuonyesha kazi zile zile, na ishara zile zile, Mathayo 28 inasema hivyo, kuwa pamoja na jeshi Lake, ndani yao, akiwalinda. Wazieni Hilo, yule Jemadari Mkuu wa Neno, Mshindi, *ndani* yetu.

174 Huenda ninawaweka muda mrefu kupita kiasi, sitaki kuwachosha. Lakini angalieni, watu nyumbani wamezoea kuketi kwa saa na saa tunapofundisha. Nitajaribu kukatiza dakika chache tu. Siwataki mtoke, ninataka kuwaombea kabla hamjaondoka. Nafikiri huu ni muhimu zaidi kwenu kuliko mstari wowote wa maombi. Mnaona? Hakika ndivyo ilivyo. Sasa, laiti mngalisikiliza tu. Mnaona?

175 Yule Jemadari Mkuu wa Ushindi, aliyeshuka na kufanywa, Neno lililofanyika mwili, alilichukua Neno hilo na kumshinda Shetani kwa kila uwanja, na kusema, "Liharibuni hekalu hili, nitalisimamisha katika siku ya tatu." Na kwa nini? Daudi katika Neno alisema ya kwamba "Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu; wala sitaiacha Nafsi Yake katika kuzimu." Naye alijua ya kwamba hiyo ilikuwa ni ahadi moja ya Mungu, ya kwamba angefufuliwa, Naye akalichukua Neno hilo, na kuingia mautini, huku akijua ya kwamba Neno hilo ilibidi litimie.

176 Hakuna hata Neno moja ambalo Mungu ameahidi ila litakalotimia. Kasema, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa." Kila ahadi ni kamilifu. Na juu ya ahadi hiyo moja katika Maandiko, "Sitamwacha Mtakatifu Wangu, aone uharibifu, sitamwacha aone uharibifu; wala sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu . . . "

177 Sasa, Yesu alijua ya kwamba uharibifu huingia mwilini baada ya saa sabini na mbili, pua hubonyea ndani, mzishi, kama yupo, angejua hilo. Sasa, uharibifu unaingia mwilini, naye Daudi alisema, kwa Roho Mtakatifu, mtu, aliyevuviwa, Neno la Bwana likimjia nabii huyu, kasema, "Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu." Naye alijua kabla seli moja haijaharibika, Yeye angefufuka kutoka kaburini.

178 Kwa nini? Yeye alikuwa ni Neno, alikingwa kwa ngome ya Neno. Naye akafufuka, akashinda mauti, kuzimu, na kaburi, na, Mwenyewe, akarudi katika umbo la Roho Mtakatifu kuliwekea ngome jeshi Lake kwa ajili ya siku hizi za mwisho, katika mashambulizi haya makubwa, ambapo hawa mabingwa mashuhuri wa kielimu wanainuka, wakitoa hoja dhidi ya Neno, lakini "Sitawaacha yatima, nitakuja tena, nami nitakuwa pamoja nanyi, ndani yenu."

179 Tena, Yeye alisema, "Nitamwomba Baba, Atawatumia Mfariji mwingine, ambaye ni Roho Mtakatifu. Atakaa nanyi

milele." Ni kitu gani? Neno, Silaha ya Mungu ndani ya mwanadamu, ikidhihirisha ufufuo, wazia hilo, yule Mshindi mkuu, aliyeshinda kila ugonjwa, akashinda kila ushirikina, akashinda kila jitu, alishinda kila kitu kilichokuwepo cha kushindwa duniani, akafa, akashinda kuzimu, akashinda mauti, akashinda kaburi, akashinda angahewa, akapaa Juu, akarudi katika umbo la Roho Mtakatifu. Nasi ni zaidi ya washindi kwa Yeye atupendaye. Amina.

180 Ni jeshi la jinsi gani! Kama vile jeshi lenye nguvu, askari Mkristo anatembea. Amina. Ushindi Mkuu, Yeye yuko ndani yetu. Si mimi, Yeye tayari ameushinda, hainibidi, kufanya jambo ila kumwamini tu na kuendelea mbele. Naam, bwana. Kwa kuwa amefufuka, Roho Wake yuko ndani yetu, yule Mshindi mkuu, Uwepo wa ufufuo uko ndani yetu.

181 Tumefufuliwa kutoka kwa mambo ya ulimwengu, kutoka kwa kutokuamini na kanuni za imani hadi kwa Kristo aliye hai, mnaona, huku kila nguvu za adui zimeshindwa. Hata mauti yenyewe imeshindwa, kuzimu imeshindwa, kaburi limeshindwa, kila ugonjwa umeshindwa. Amina. Sio, mimi mshindi, Yeye alishinda. Si kile nilicho mimi, kile Yeye alicho. Amina. Yuko wapi? Ndani yangu. Nilipita kutoka mautini kuingia Uzimani.

Mtu fulani alisema, "Billy, unatenda kijinga."

182 Vema, labda ndivyo nilivyo, lakini ninajisikia vizuri zaidi hivi, niacheni tu. Hiyo ni kweli. *Hapa* ndani nina Uzima, *huko* nje nilikuwa nimekufa. Mimi ni bora zaidi nikiishi leo. Amina. Loo, ninalipenda! Haendi mbele yetu, Yeye anaenda ndani yetu.

183 Moto mkubwa ulizuka huko Jeffersonville, hapa si muda mrefu uliopita. Jeshi la Pfau, ama, kampuni hiyo ikaanza kuteketea, nao wakaagizia na kukichukua kikosi cha zimamoto. Huku Kikosi cha Zimamoto cha Jeffersonville kimesimama kama mvulana mwenye bomba dogo, yule chifu akitembea pale na msokoto kama maksai wa Teksas aliyeng'olewa pembe, akitembea pale akisema, "Bubujisheni maji kidogo *hapa* juu." *Puuf*, *puuf*, *whiu! Puuf*, *puuf*, *whiu!* "Bubujisheni maji kidogo *hapa* juu, enyi wavulana. Hima, hima!" Kila mtu anaona alikuwa ndiye chifu. "Bubujisheni maji kidogo *hapa* juu."

184 "Vema," wakasema, "inatubidi kuita idara nyingine ya zimamoto. Yeye, wao hawatoshi." Wakatuma mtu Clarksville, hawa hapa wanakuja, *bang*, *bang*, *bang*. Wakapanda kule juu, naye chifu huyo akatoka nje, akapeana mikono na yule chifu mwingine, wakitoa heshima mmoja kwa mwingine.

185 Nawe unawezaje kuwa na imani, wakati mnaheshimiana? *Brrrrr*, jamani! Ati mtu fulani mashuhuri, askofu, jamaa mkubwa mno, mzee wa jimbo: Bure! Sisi ni ndugu na dada katika Kristo Yesu, hakuna kitu kikubwa miongoni mwetu, ni Kile kilicho ndani yetu ndicho kikubwa, Mungu, Roho Mtakatifu, ndani ya kila mmoja wetu aaminiye. Hakuna

maaskofu wakuu watakatifu na baba watakatifu, ni Roho Mtakatifu aliye ndani ya watu. Naam.

186 Kwa hiyo kikaja hiki Kikosi cha Zimamoto cha Clarksville, "Habari za jioni, Askofu, ha, ha." Naam, namna hiyo. Jengo likaendelea kuteketea moja kwa moja.

187 Baada ya kitambo kidogo wakapiga simu Louisville. Ndugu, walikuwa na kitu fulani wakati huo. Ninaweza tu kusimama pale sasa na kuona maskini kiopoo hicho cha kale na ngazi ikivushwa pale. Nao wakienda pale, wakisema, "Livunjeni *hilo* dirisha. Bubujisheni maji kidogo *huko* ndani."

188 Wakati hilo jeshi kubwa la wapiganaji lililofunzwa la Louisville lilipokuja pale, walilizungushazungusha upesi lori hilo pale mtaani, ndugu. Wakafagia nusu ya kijinjia walipogeuka. Ni nani aliyekuwa mwishoni mwa ile ngazi? Walikuwa na lifti ya mtambo iliyoirusha juu. Ni nani aliyekuwa mwishoni mwa ile ngazi? Mkuu wa zimamoto mwenyewe. Amina. Wakati wao. . .Alikuwa na bomba mkononi mwake na shoka kwenye mkono huo mwingine, kasema, "Iachilie." Nao wakauvuta huo wenzo.

189 Ni nani aliyetangulia? Mkuu wa zimamoto. Wakati ilipougonga ukuta, alichukua shoka hilo kabla ngazi haijaegemea ukutani, na kuligongesha kupitia hilo dirisha, kasema, "Haya njoni, enyi wavulana!" Sio, "Endeleeni, enyi wavulana." "Haya njoni, enyi wavulana!" Haleluya! Hivyo ndivyo Kristo alivyofanya. Neno lilikuja, likaishi kama mwanadamu, likashinda mauti, kuzimu, kaburi, kamwe hakusema, "Endeleeni." Alisema, "Hima njoni, niko pamoja nanyi." Hmm! Moto ulizimika upesi sana.

190 Hivyo ndivyo ilivyo, yule Mshindi mkuu. Hatuhitaji madhehebu makubwa mno ya kielimu, "Mimi ni mfuasi wa kanisa lililo kubwa kuliko yote mjini." Upuuzi. Mimi ni mfuasi wa Lile lililo dogo kuliko yote, bali hilo Ndilo.

191 Nimekuwa katika familia ya Branham kwa miaka hamsini na mitatu, kamwe hawakuniomba nijiunge na familia hiyo. Nilizaliwa Branham. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo ulivyo mwana wa Mungu, unazaliwa mwana wa Mungu kwa kuzaliwa upya. Chifu akiongoza katika kila vita; Chifu wetu mkuu akiongoza njia ya kurudi Nyumbani.

192 Wakati mataifa. . .Sikilizeni sasa, katika kufunga. Wakati mataifa, hapa si muda mrefu uliopita, yalipoanza kutoa chapeo kwa ajili ya ulinzi wa jeshi lao, sasa, walijua itawabidi kuitumia, walijua kutaruka maganda ya risasi, kwa hiyo walijua iliwabidi kuzitumia. Loo, huenda haikuonekana ni muhimu sana wakati wakifunzwa, lakini ndugu, mara wakiwa kwenye uwanja wa vita, inakubidi kuwa nayo.

193 Wanapowafunza askari, kama kuna yeyote hapa, nafikiri ni kifurushi cha ratili tisini wanachoweka kwenye mgongo wa

maskini kuruta. Anaanzia hapa nje, na karibu atokwe na jasho hata kufa. Anapofunzwa yeye hafikirii ni muhimu, bali ngoja tu mpaka wakati utakapowadia, atahitaji kila kitu kilicho kwenye kifurushi hicho, atafurahi alikuwa nacho. Naam, bwana. Ha—hana budi kuwa nacho, naye atafurahi kwamba walimfundisha kukitumia.

194 Na kwa hiyo sasa, Mungu, akijua ya kwamba siku hizi za mwisho watakuja mabingwa wa kielimu, kutakuja kila kitu cha kiakili, adui wa kila namna hodari wa kutoa hoja kujaribu kulithibitishia Kanisa ya kwamba siku za miujiza zimepita na haya yote, Mungu amepakia katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, na nini? Kunena kwa lugha, kufasiri lugha, unabii, karama, na mambo ya kila namna. Huenda yakaonekana ni magumu katika mafunzo, lakini, ndugu, kwenye mstari wa mbele wa vita, kila moja la hayo halina budi kutumiwa. Mungu huwaandaa askari Wake na yale hasa yanayohitajika kutumika. Amina.

195 Loo, huenda wakasema, "Jifunze tu saikolojia." Hiyo haitafaa kitu. La, bwana. Hiyo ni nyembamba kama mchuzi uliotengenezwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa. Basi hiyo haifai kitu. Hatuna budi kuwa na nguvu za Roho Mtakatifu zikija juu ya mwanadamu, huku zile karama zote tisa za kiroho zikikaa ndani yake.

196 "Loo," unasema, "Kamwe sipendi kushuka kwenda kule. Sipendi kuomba usiku kucha. Sipendi kuninii. . . " Vema, basi utauawa huko nje kwenye mstari wa mbele wa vita. Wewe kaa hapo mpaka Mungu atakapokuandaa kwa ubatizo wa Roho, ndipo kila kitu unachohitaji katika ulimwengu huu ama Ulimwengu ujao, kinaishi moja kwa moja ndani yako. Mungu mwenye hekima yote alijua jinsi ya kuliandaa jeshi Lake. Aliliandaa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, huo ndio hasa alioutuma kwa ajili ya siku hizi za mwisho.

197 Alijua ya kwamba ingetubidi kuwa nao, alijua ya kwamba watu wangetoa hoja, wangeanza kusoma Neno hili wakati litakapochapishwa hapa, jambo ambalo lingetukia. Na siku hizi tunaona watu wakisema, "Vema sasa, yuko wapi yule Mungu wa historia? Yuko wapi Mungu yule aliyevuka Bahari ya Shamu? Yuko wapi yule Mungu aliyewaponya wagonjwa?" Wanajaribu kusema, "Ni huko nyuma."

198 Inafaa nini kuwapa kurumbizi wako vitamini, na kumfanya awe na mabawa mazuri yenye nguvu, kisha kumweka kizimbani? Kile wanachojaribu kufanya na watu, kuwalisha kila namna ya vitamini za *hiki*, *kile*, na *kinginecho*, na muda si muda mwajua, kuwaambia siku zote za miujiza zimepita, umefungiwa kwenye kitu kidogo *hapa* chini. Ni uongo! Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mungu alijua ingehitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu kuthibitisha ishara Zake za siku za mwisho, hiyo ni kweli, Alijua, kuwa shahidi afaaye.

199 Kama vile rafiki yetu mpendwa, silitaji jina lake, kwa sababu si vizuri, huu unarekodiwa kwenye kanda, bali ni rafiki wa thamani, ndugu mzuri, yule ambaye, akishuka kwenda Sodoma nilivyowaambia hivi majuzi usiku, wakati alipokuwa India, mnajua ni nani ninayenena habari zake, yule askofu wa Kihindi alimpa changamoto kwamba hakukuwako na Kitu kama Kristo, ilikuwa ni dini iliyobuniwa na mwanadamu, akasema, "Nitawaleta watu thelathini upande *huu*, wagonjwa, nawe uchukue thelathini upande *ule*. Nitamponya mmoja kila unapomponya mmoja. Nayo Biblia yako inafundisha ya kwamba itaponya."

Ndipo mwinjilisti huyu *fulani* mashuhuri akasema, "Siku za miujiza zimepita, Yeye asingefanya jambo kama hilo."

200 Nafikiri, kama Eliya alivyosema wakati ule, "Kwa nini hukutuma? Kama hukuwa na imani ya kufanya hivyo, kuna wengi wa hao hapa walio nayo." Loo, ndugu, huenda nimeshindwa, lakini kamwe nisingemwacha huyo kafiri asimame hapo, ama, huyo asiyeamini, na—na kulidhihaki Neno la Mungu, kama ingenibidi kushindwa, ningalishindwa nikilitumainia Neno la Mungu.

201 Kama vile wana wa Kiebrania walivyosema, "Mungu wetu anaweza kutuokoa na moto huu, lakini, hata hivyo, kamwe hatutakubali kanuni hizi za imani." Hiyo ni kweli.

202 Unahitaji Roho Mtakatifu kusukuma huko nje. Kwa nini hakusema hivyo tulipokuwa India? Kwa nini hakusema hivyo wakati yule kipofu alipokuja moja kwa moja mbele ya Mfalme Nehru pale, na kuja mbele za hao watu, na kushuhudia kuwa kipofu kabisa katika seminari ya Kimethodisti, naye akaponywa, na kufanywa mzima kabisa jukwaani. Wanajua la kutolea changamoto na lipi wasilitolee, bila shaka wanajua. Wanafikiri wana nafasi.

203 Shetani anajua hoja hiyo na mahali hoja ilipo. Naam, bwana. Kuwa shahidi afaaye wa kufufuka Kwake, Alijua ingehitaji Roho Mtakatifu, maana mwanadamu hawezi kufanya mambo hayo. Aliliandaa jeshi Lake kwa Roho Mtakatifu kufanya mambo hayo, kutambua siri za moyo, kama alivyoahidi. Huwezi kufanya hivyo kwa mafunzo ya aina yoyote, huna budi kufanya hivyo kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, Silaha za Mungu, na hii ndiyo Nuru ya jioni.

204 Kufanya Waebrania 13:8 halisi, ingehitaji zaidi ya mafunzo. Unaweza kusoma maneno, na kusoma maneno, na kusoma maneno, wala kamwe haitalifanya litimie mpaka uwe na Roho Mtakatifu pale kulidhihirisha hilo. Hiyo ndiyo Nuru.

205 Kuvaa silaha zote za Mungu, si mavazi tu, kuvaa na kusema, "Utukufu kwa Mungu, ninaye Roho Mtakatifu." Basi unabubujisha nguvu zote kwa filimbi, hufai kitu. Liweke katika matendo, liweke katika imani, lifanye litende kazi, lifanye

litende jambo. Kuvaa Silaha zote za Mungu kutoka nje na kuzipinga hila za ibilisi!

206 Wakati aliposema, "Yesu Kristo ni dini bandia, imekufa kwa muda mrefu. Hakuna kitu kama *hiki*, hakuna kitu kama *hicho*, na siku za miujiza zimepita," simama hapo pamoja na ubatizo wa Roho Mtakatifu na kuthibitisha kwamba ni kweli. Utukufu! Hmm!

207 Mnafikiri ninatenda kiajabu? Labda natenda. Nimepoteza akili zangu kwa ulimwengu, na kuzipata katika Kristo, "Nia iliyokuwamo ndani ya Kristo na iwe ndani yenu."

208 Inahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu, Silaha zote za Mungu, sio tu kupeana mikono na mhubiri, kuandika jina lako kwenye kitabu, ama kuchukua mkate mwembamba na kuumeza, kisha kuhani anywe ninii . . . divai, hilo silo. Lakini, ndugu, ni kukaa hapo mpaka uje Upepo wenye nguvu ukienda kasi unaoujaza utu wako wote, unaondoa mashaka yako yote, unaondoa kanuni zako zote za imani, unaondoa chochote kile, na kuliweka Neno mle ndani pamoja na nguvu za Mungu nyuma Yake kuliunga mkono. Utukufu! Ninajisikia vizuri sana. Amina. Mungu alisema hivyo. Ni Roho Mtakatifu, si . . .

209 Nina mengi zaidi hapa, bali sitayasema. Ndugu, Silaha zote za Mungu ni ubatizo wa Roho Mtakatifu pamoja na Neno nyuma yake. Na kama mtu yeyote akisema wanaye Roho Mtakatifu na kukana Neno moja la *Hii*, basi si Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu aliiandika Biblia hii, Naye akasema, "Mtu yeyote atakayeondoa lolote kutoka Kwake, ama kuweka lolote ndani Yake, huyo ataondolewa, sehemu yake kutoka kwenye Kitabu cha Uzima." Roho Mtakatifu hutambua Neno pekee, kwa sababu hilo ni Neno Lake, wala hawezi kulighairi Neno Lake, hana budi kulitimiza Neno Lake. Amina.

210 Mtu fulani alisema, "Tunaye Roho Mtakatifu, wala hatuamini miujiza." Basi inathibitisha hunaye Huyo. Amina. Mtu yeyote ambaye angeziita nguvu za Mungu, za upambanuzi, na manabii, na kadhalika, katika siku za mwisho, telepathia ya—ya kiakili ama chochote kile, amezaliwa na ibilisi. Haliwezi kuwa ni la Mungu, ni kinyume, halitambui Urimu na Thumimu. Chochote kinacholitambua *Hili* na kumulika nyuma, "Kweli," ni Mungu. Amina.

211 Loo, ninampenda. Yuko hapa. Maskini Neno Hilo, hakuna kitu kinacholeta imani kama Neno. Silaha zote za Mungu, askari waliofunzwa!

212 Yesu alisema hapa ndani, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Hiyo ni kweli? Alijitambulishaje, Masihi? Kwa kuweza kuyatambua mawazo yenyewe yaliyokuwa niani mwao. Yeye alilinenaje katika Agano Jipya? "Kazi zile zile nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Waebrania, mlango wa 4, Yeye alilichukua tena, kasema, "Neno la Mungu ni kali

kuliko upanga ukatao kuwili, likichoma hata mafuta ya mfupa, na viungo," na kadhalika, "na Huyatambua mawazo yaliyo moyoni." Haleluya!

213 Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za—za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu," wakati Mungu alipojitambulisha Mwenyewe katika Mwanadamu, akageuza mgongo Wake, namna *hii*, kwa kusanyiko, naye alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwa mwanamke, na kumwambia kile alichokuwa akiwazia akiwa ndani. Hilo ni Neno la Mungu, ni kweli ya Mungu.

214 Watu, huenda mkawazia, maana tumeketi hapa maskini watu mia nne ama mia tano, tumeketi humu jengoni alasiri ya leo, ni wachache sana. Kumbukeni, Mungu kamwe hakusanyiki katika umati mkubwa, "Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa katikati yao." Hilo halimaanishi, unasema, "Vema, tumekusanyika katika Jina la Yesu." Hiyo inamaanisha kwamba wewe kweli uko ndani ya Kristo. Ulimwengu umekufa kwako, nawe umekufa kwa ulimwengu, naye Kristo yu hai ndani yako.

215 Yuko hapa bila shaka lolote. Ninamwona akitembea kwenye kusanyiko sasa. Amina. Ananisimamisha. Wewe amini tu.

216 Vipi kukuhusu wewe, Mama? Sikujui wewe unayeketi hapo. Una wasiwasi, matatizo, ugonjwa wa matumbo. Unaamini Mungu alikuponya? Inua mkono wako kama utaukubali. Nenda zako.

217 Mama aliyeketi moja kwa moja nyuma yake hapo. Naam. Kidonda. Kama unaweza kuamini, Mungu atakupa afya. Usitilie shaka, amini kwa moyo wako wote naye Mungu ataondoa hicho kidonda. Unaamini? Kiko kwenye mguu wako wa kulia. Amini kwa moyo wako wote. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema.

218 Simjui mwanamke huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu. Kama hatufahamiani, punga mkono wako namna *hiyo*. Mnaona? Ni kitu gani? Ni Kristo, Silaha zote za Mungu. Sikilizeni, Neno ni Upanga, na kuna kitu kimoja tu kinachoweza kupigana na adui, hicho ni mkono wa imani kuushika huo Upanga.

219 Hapa si muda mrefu uliopita mtu fulani alisema aliota kwamba ibilisi aliendelea kusema, "Buu! Buu!" Naye angeruka nyuma, naye ibilisi angekuwa mkubwa zaidi naye angekuwa mdogo. Alijua ilimbidi kupigana naye, kwa hiyo akalinyakua Neno, na kila wakati ibilisi angesema, "Buu!" yeye alisema, "Buu!" moja kwa moja tena, naye ibilisi akawa mdogo. Hivyo ndivyo ilivyo. Inahitaji mkono wa imani kushikilia Neno la Mungu. Haleluya!

Na wewe je? Unaye jamaa, ana kiharusi. Hiyo ni kweli, sivyo? Naam. Unaamini atapona? Kuwa tu na imani.

Mnasema, "Ulikuwa ukimwangalia." Vema.

220 Kuna mwanamume na mwanamke wameketi nyuma yangu. Mwanamume huyo ana ugonjwa wa damu, yabisi kavu. Mkewe ameketi karibu naye, ana ugonjwa wa kikoromeo. Bibi na Bw. Rader, aminini kwa moyo wenu wote, na Mungu atawaponya, mkitaka kuamini. Nawe je, Bwana?

221 Mimi siwajui. Kama hatufahamiani, mmoja kwa mwingine, inua mkono wako. Mnaona? Haya basi. Ni kitu gani? Silaha zote za Mungu. Haleluya!

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu . . .

222 Hilo lilikudumaza, Bwana. Hukujua ulikuwa na imani kiasi hicho. Lakini nilikuwa nimesimama hapa nikiangalia Nuru hiyo ikizunguka, Nikawaza, "Kama nikigeuza mgongo wangu watamwona Malaika yeye yule aliyeishi kule nyuma, kisha akashuka na kujidhihirisha Mwenyewe, na kusema yale hao watu waliyokuwa wakiwazia hemani, hakika angeweza kujua wewe ulikuwa ni nani, na shida yako."

223 Ninampa changamoto mtu yeyote humu ndani kuamini jambo lile lile. Haleluya! Nguvu za Mungu, Silaha zote za Mungu, Neno lote la Mungu limefungiwa ndani yako; yule Mshindi mkuu.

224 Loo, "Yeye ndiye Mshindi Mwenye Nguvu tangu alipopasua lile pazia vipande viwili." Hiyo ni kusema, si mtu mmoja tu, bali kila mtu, yeyote atakaye, anaweza kuja nyuma ya Pazia sasa, aonje na kusimama katika Utukufu wa Shekina. Amina. Akawa ukuhani wa kifalme.

225 Walipoenda huko nyuma, wangeweza kuonja ambapo walikuwa na chungu kilichojaa, pishi asili, iliyojaa ma—mana iliyoanguka hapo mwanzo, iliwekwa mle ndani tu kwa ajili ya ukuhani, tunajua hilo. Lakini sasa pazia limepasuliwa, sio tu ukuhani, bali kila mmoja wetu anaweza kuwa makuhani wa kifalme.

226 Ingia ndani na kuonja ile Mana ya asili, kama ile iliyoanguka kwenye Siku ya Pentekoste, ile Mana kwa ajili ya Kanisa, Roho Mtakatifu, Silaha, kile tulichoimarishiwa si kwa elimu ya kiakili, digrii ya udaktari, bali tumeimarishwa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu kuthibitisha Neno la Mungu ni kweli. Utukufu! Haleluya! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo?

227 Hebu na tumwimbie, "Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza." Kila mtu sasa.

> Nampenda . . .

Je, unampenda? Inua mkono wako.

> . . . nampenda

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalvari . . .

Hivi hamna furaha? Hivi hamna furaha? Tupe *Twendeni, Askari Wakristo*, Ndugu, katika kutembea taratibu, 4/4 tafadhali. Vema. Loo, jamani! Loo!

Tukienda kama vitani,
Loo, pamoja na msalaba wa . . .

Hebu na tusimame sasa.

. . . Yesu
Ukitangulia;
Kristo, Bwana wa kifalme,
Loo, anaongoza dhidi ya adui; (Tuna nini? Silaha.)
Twendeni vitani,
Angalieni bendera Zake zikiondoka!

Twendeni askari Wakristo!
Tukienda kama vitani,
Huku msalaba wa Yesu
Ukitangulia.

228 Humwonei haya, sivyo? Paulo alisema, "Siionei haya Injili ya Yesu Kristo, kwa kuwa ni nguvu za Mungu ziletazo wokovu." Hebu na tuchukue tu mikono yetu na kusema, "Haleluya!" kwa sauti kubwa sana, sasa. Hima. "Haleluya! Haleluya! Haleluya!" Mungu wetu asifiwe. Mungu wetu asifiwe.

. . . jeshi
Kanisa la Mungu linatembea;
Ndugu, tunakanyaga
Loo, ambapo watakatifu wamekanyaga;
Loo, hatujagawanyika,
Loo, sisi sote mwili mmoja;
Loo, mmoja katika tumaini na mafundisho,
Mmoja katika upendo.

Kila mtu sasa, uimbeni.

Twendeni, askari Wakristo!
Tukienda kama vitani,
Loo, huku msalaba wa Yesu
Ukitutangulia.

229 Je, ungependa kujiunga? Njia pekee unayoweza kujiunga ni kuzaliwa. Sasa, kitu hicho kikuu kimefunguliwa hapa, madhabahu ya Mungu, kuna nafasi kwenye chemchemi. Mtu yeyote hapa ndani angetaka kujiunga na makundi haya alasiri ya leo, ambaye ataweka kando kila kanuni ya imani ambayo ni kinyume na Biblia, kila wazo ambalo ni kinyume na Biblia, kila fundisho ambalo ni kinyume na Biblia, na kwa imani aje hapa na kusema, "Ninamkubali Yesu Kristo juu ya msingi wa Damu

Yake iliyomwagika na Neno Lake," nakwambia jambo fulani litakufanyikia papa hapa, nawe utalindwa kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

230 Hakuna mtu aliye na haki ya kudai kwamba yeye ni mhubiri mpaka aupate huo mchanga mtakatifu. Musa alikuwa mwenye akili tu kadiri alivyoweza kuwa, alikuwa na nguvu za, uh, maarifa ya Neno, alijua mahali pake, alijua alikuwa ni nabii, kila kitu, lakini mpaka alipokutana na Mungu kwenye mchanga huo mtakatifu huko nyuma . . . Hakuna mwenye elimu angaliweza kuliondoa kwake kwa maelezo, yeye alikuwako wakati lilipotukia.

231 Hakuna mtu aliye na haki ya kudai Mungu mpaka umefikia mahali hapo patakatifu, ambapo hakuna bingwa wa kielimu anayeweza kugusa kamwe, ulikuwapo wakati lilipotukia, haileti tofauti, kile wanachoweza kuelezea, unajua lilitendeka. Loo, utukufu!

232 Je, mnataka kujiunga nasi tunapouimba huu mara nyingine tena? Njoni madhabahuni, tungefurahia kuwaombea kabla hatujaanzisha mstari wa maombi. Vema, Ndugu, tena, *Twendeni, Askari Wakristo*. Njoo sasa, jiunge nasi. Wito wa mwisho. Ukitaka kuja, njoo sasa.

Twendeni, askari Wakristo!
Tukienda . . .

Kama hujaimarishwa na Roho na Neno!

. . . Yesu
Akitutangulia.
Kristo, Bwana wa kifalme, (Mshindi Mkuu!)
Anaongoza dhidi ya (Kutokuamini!) adui (Hoja!);
Twendeni mbele vitani,
Angalieni bendera Zake zikienda!

Twendeni askari Wakristo!
Tukienda kama vitani,
Loo, huku msalaba wa Yesu
Ukitutangulia.

233 Ni wangapi hapa ndani tayari wako katika jeshi hilo, tayari wamejazwa na Roho Mtakatifu, wakiamini kila Neno la Mungu, wanajua ya kwamba ni kweli?

234 Baba yetu wa Mbinguni, sijui ni lini nitakapoweza kurudi kwenye pwani hii tena kuwaona watu hawa, natumaini hivi karibuni tena. Lakini, Baba wa Mbinguni, ninakushukuru kwa ajili ya ushuhuda huu mkuu, usiku baada ya usiku, mwujiza baada ya mwujiza wa Mungu asiyejulikana na asiyeonekana, anatenda kazi miongoni mwa watu, pamoja na mambo yasiyojulikana ambayo hawajui kitu juu yake, kumwona Yeye akijidhihirisha Mwenyewe, na kuufanya Utu

Wake ujulikane hapa, akithibitisha ya kwamba hajafa bali amefufuka kutoka kaburini.

235 Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utawapa watu hawa nguvu zote za uweza wa Roho Mtakatifu, ili waweze kuwa mashahidi huku na huku pwani hii, katika siku za mwisho. Kwa kuwa kweli, Bwana, mtu yeyote aliye na hali nzuri ya akili anajua ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho, kila msomaji wa Biblia anajua jambo hilo, ulimwengu unajua jambo hilo. Wanasayansi wanasema ya kwamba tuko dakika tatu kabla ya usiku wa manane, saa ya kushangaza imewadia.

236 Nawe uliahidi, ya kwamba katika siku hii, kile kingetukia. Tunasoma katika Kitabu cha Ufunuo, kwenye Wakati huu wa Kanisa la Laodikia, ambapo wale mabingwa wa kielimu waliingia na kumsukuma Kristo moja kwa moja kutoka kanisani Mwake, Naye alikuwa amesimama akibisha mlango wa nyumba Yake Mwenyewe akijaribu kurudi ndani. Ee Mungu, si mwingine, ama wakati mwingine iliwahi kuwa hivyo, bali ni katika wakati huu, wakati huu wa kielimu.

237 Lakini umewavika askari Wako, Bwana, kinga, ngao, chapeo, Neno, nasi tunasimama alasiri ya leo kama kundi katika uchache, lakini, Ee Mungu, tuchonge, tufanye, tunyoe, tuondolee kutokuamini na mambo ya ulimwengu, hata Kristo atakapokuja Yeye atatoshea moja kwa moja katika Kanisa Lake kikamilifu, katika mpango Wao, kwa kuwa utakuwa ni mpango wa Roho Mtakatifu, ukiongozwa, na kuendelezwa, na matendo ya Roho Mtakatifu wakati Kristo atakapokuja. Tujalie, Baba, katika Jina la Yesu naomba. Amina.

238 Mnaweza kuketi kwa muda kidogo tu. Nitamwomba kila mtu sasa, walio na kadi za maombi . . . Wakati, kwa kawaida, mwinjilisti anapoingia mjini, wanakuta, wanasema, "Vema, mhubiri tu, ngoja mpaka Ndugu Branham, Ndugu Roberts, mtu fulani." Haihitaji hiyo, inawachukua watu hawa pia. Nitawaomba wanisaidie kuwaombea wagonjwa alasiri ya leo, mtaona jambo fulani likitukia pia. Vema.

239 Vema. Ni wangapi walio na kadi za maombi? Inua mkono wako. Vema, ninawatakeni mpange mstari moja kwa moja upande huu, moja kwa moja kwenye marefu haya ya kanisa hapa, kisha mje moja kwa moja huku, kila mtu aliye na kadi za maombi. (Fanyeni hivyo baada—baada ya sisi kuanza. La, nitawachukua sasa hivi pamoja na kadi zao kwanza.) Sasa, pangeni mstari papa hapa. Nawataka ndugu zangu waje hapa pamoja nami. (Ninii tu, nyote mtawaombea.)

240 Biblia ilisema, Yesu alisema, na Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Lake haliwezi kushindwa. Sasa, sikilizeni kwa makini, enyi marafiki, kama hamwamini jambo hili, mnatembea tu katika mkondo huo usio na matokeo. Ninataka kuwaulizeni, kutoka katika mambo mengi, mengi sana ambayo Roho

Mtakatifu ametaja juu ya kanisa juma hili, je, amekosea katika lolote la hayo? Kuna mtu yeyote aliyewahi kumwona akikosea katika mikutano mingine? Je, amekuwa mkweli daima? Kama ndivyo, inueni mikono yenu. Daima ni kweli. Mnaona? Vema. Basi Roho Mtakatifu yuyo huyo yuko papa hapa.

241 Maskini mwanamke huyo aliyeketi hapa muda mfupi uliopita, hapa chini mahali fulani, alikuwa na imani ya kutosha kwa ajili yake na mumewe. Sikumbuki, ilionekana kama ndoto kwangu kwa namna fulani. Vema. Kama una imani kwa baadhi ya wapendwa wako, waombee wakati wakiwa kwenye mstari huu.

242 Sasa, tutawaombea hawa kwanza, tuliahidi hilo. Na sasa, mnapopitia kwenye mstari huu, hawa hapa watu hapa wenye mamlaka kama mtu mwingine yeyote alivyo nayo kuwaombea wagonjwa.

243 Sasa sikilizeni, ninawatakeni nyote, mnukuu Maandiko haya pamoja nami. Yesu alisema hivi katika agizo la mwisho alilolipa Kanisa Lake, baada ya kuwatokea wale kumi na mmoja na kuwakemea kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao na kutokuamini kwao, kwa sababu hawakuwasadiki wale waliomwona baada ya kufufuka Kwake, aliwaambia, "Enendeni ulimwenguni kote . . ." Sasa, kumbukeni, Yeye anatwaliwa juu sasa. "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa." Hiyo ni kwa wote watakaolisoma, "Na . . ." *Na* ni kiunganishi kinachounganisha sentensi pamoja. "Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio . . ."

244 Mmefundishwa, "Wanapeana mikono, na kuandika jina lao kwenye kitabu." Yesu alisema tofauti, Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; wakishika nyoka ama wakinywa kitu cha kufisha hakitawadhuru; na wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya."

245 Hilo ndilo agizo la mwisho alilotoa Yesu, na hili hapa swali alilouliza: "Je, nitaikuta imani nitakaporudi?" Sasa, Yeye kamwe hakusema, "Je, nitaikuta haki? Nitakuta kanisa? Nitakuta watu?" Alisema, "Je, nitaikuta imani?" Hilo ndilo swali.

246 Sasa, kwenu ninyi mnaokuja kwenye mstari huu wa maombi, wazee hawa na watu wanaosimama hapa, Wakristo, waliojazwa na Roho Mtakatifu, wanaenda, pamoja, pamoja na mimi mwenyewe, tutamwekea mikono kila mtu anayepitia hapa, nawe unajua ya kwamba utaponywa. Toka moja kwa moja hapa na kusema, "Ni sawa, nitakuwa mzima." Hilo latosha.

247 Sasa, mstari huu utakapokwisha, basi tutaita sehemu baada ya sehemu, mpaka kila mtu aombewe anayetaka kuombewa, niliahidi jambo hilo.

248 Ni wangapi huko nje watakuwa wakiuombea mstari huu wa maombi? Inueni mikono yenu. Vema. Ndugu, kwenye kinanda, tupe ule wimbo *Amini Tu* sasa, na tuombe sasa, kila mtu. Nawe ndugu, dada, simama moja kwa moja mahali ulipo, usimruhusu mtu apite bila kuwawekea mikono.

249 Mleteni mtu hapa, sasa, anayeweza kuwasaidia watu jukwaani, mtu fulani anayeweza kuwasaidia. Njoo hapa, Ndugu Fred, tafadhali. Ndugu Fred Sothmann pale, mmoja wa wadhamini wangu, njoo hapa na—na uwasaidie watu watoke jukwaani wanapokuja, simama papa *hapa*. Pia mtu fulani ashuke kule chini kusaidia kule chini. Au wana...? Wanao, naam, wanao mabawabu kule chini. Sawa. Vema, hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

250 Baba yetu wa Mbinguni, tuko hapa kukusaidia. Nasi tunatambua, tunapowahudumia watoto Wako, Wewe ulisema, "Kadiri mlivyowatendea walio wadogo sana wa hawa waniaminio Mimi, mmenitendea Mimi." Sasa, hawa hapa mama, baba, wapenzi, watoto, wamesimama kwenye mstari huu hapa, watoto wachanga, nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba wakati sisi, katika njia yetu nyenyekevu, pamoja na yote tunayojua jinsi ya kuwafanyia watu, ni kulihubiri Neno, kulielezea kwao, ndipo tunakuona Wewe ukishuka na kuyatambua mawazo ya watu, ukithibitisha ya kwamba Wewe upo hapa, hiyo inakufanya Wewe Nguzo kuu ya Moto, Kristo mkuu wa Mungu, yeye yule jana, leo, na hata milele.

251 Basi hawa watu waliotiwa mafuta, pamoja na Roho Wako, wamesimama hapa kuwawekea wagonjwa mikono. Mungu, twaomba ya kwamba kusiweko na asiyeamini hata mmoja miongoni mwao, na kila mtu anaweza kutoka hapa akiwa na furaha, akishangilia, na kuona ugonjwa na mateso ya miili yao yakitoweka. Tujalie, Baba. Tunawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu. Amina.

252 Sasa, ninataka kiongozi mmoja wa nyimbo, anayeweza kuongoza nyimbo. Njoo hapa, Roy. Ninataka kila mtu huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa, katika maombi, huku ukiimba moyoni mwako, "Amini tu, mambo yote yanawezekana," huku Ndugu Borders akiuongoza huo wimbo. Kila mtu aanze kuomba sasa tunapoomba. Sasa kila-...

Amini tu...

Kila mtu akiimba sasa.

...amini tu,

[Ndugu Branham anawaombea watu. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

253 ...-mtu ameombewa sasa? Yeye si ni wa ajabu? Niliona wakipitia kwenye mistari...Sasa, kumbukeni tu, kuna watu hapa wangeweza kushuhudia kwamba wamekuwa katika

mikutano mingine, na kupita tu mstarini, waombewe, nasi tungeweza kulundika kitu hiki hapa kijae barua za ushuhuda, taarifa zilizotiwa sahihi na madaktari, kansa, kiharusi, polio, kila kitu kilichoponywa. Mnaona, lazima uitie tu nanga na kuishikilia. Usiiachilie, kaa tu papo hapo. Sasa, kumbukeni, mnaanza kuona baada ya kitambo kidogo . . .

254 Hivi majuzi tu tulikuwa na mkutano, na kulikuwa na mama aliyepitia mstarini, naye alikuwa . . . Ilimwambia kuhusu shida yake. Alikuwa na ugonjwa wa tumbo, kidonda tumboni mwake, nayo ikamwambia, "BWANA ASEMA HIVI, umeponywa." Nayo ikasema, ikamwambia aende zake nyumbani akale.

255 Ndipo mama mwingine akapita, naye alikuwa na uvimbe kando ya shingo yake *hapa*, loo, nadhani urefu wa inchi moja, ama chochote kile, na kumwambia jambo lile lile, atakuwa mzima. Na kwa hiyo walikuwa majirani.

256 Naye mama huyo aliyekuwa na kidonda cha tumbo akaendelea, akajaribu kula wala asingeweza kula. Naye angejaribu kula chakula, naye angekitapika tu. Basi hatimaye, iliendelea kwa yapata majuma mawili au matatu, naye alininii tu, alionekana kana kwamba alikuwa tu anaelekea kushindwa. Halafu tungeninii, katika sehemu nyingine ya nchi yapata majuma matatu ama majuma manne baadaye.

257 Basi asubuhi moja watoto wake walikuwa wakienda shuleni, naye akaamka. Na kila wakati angekula chochote angeninii tu, angeshikwa tu na mchomo na kuumwa, naye angetapika tu. Ndipo hatimaye, mumewe akasema, "Mpenzi, ni—ninaamini unaleta shutuma juu ya huduma ya Kristo."

258 Sasa, huwezi kufanya hivyo wakati unapokiri. *Kukiri* maana yake ni "kusema jambo lile lile." Kukiri, unapoenda kwa wakili, ama ku—kukiri, unasema jambo lile lile. Nawe unasema, "Kwa kupigwa Kwake mimi nimepona." Hivyo ndivyo alivyosema, nawe unakiri ya kwamba amefanya jambo hilo. Basi akaendelea.

259 Kwa hiyo asubuhi moja alikuwa amesimama pale akiosha vyombo, akilia. Naye, mara akashikwa na hisia ndogo ya ajabu, akasema, ikamjia, ndipo tumbo lake likaanza kuingia baridi. Vema, kamwe hakulitambua, aliendelea tu kuosha vyombo, akashikwa na njaa sana. Huyo mwanamke huenda ameketi hapa sasa, nijuavyo mimi. Naye akasema watoto walikuwa wameacha shayiri kwenye sahani yao, mwajua, shayiri iliyokunjwa, mwajua, iliyopikwa, na kwa kawaida hiyo ilimchoma tu, kwa kidonda cha tumbo. Kwa hiyo akachota kijiko kimoja ama viwili, wala haikumsumbua.

260 Halafu basi, baada ya kitambo kidogo akala kipande cha tosti, hakikumsumbua. Kwa hiyo basi, alijikaangia tu mayai kadhaa, na kuchukua kikombe cha kahawa, ndipo akawa tu na yubile ya kawaida ya kula chakula. Alikula tu moja kwa moja,

hakikumsumbua. Naye akangojea yapata saa mbili ama tatu, hakuna kitu, hakuna madhara.

261 Akakimbia kwenda kwa jirani yake kumwambia jirani yake, naye jirani yake alikuwa akipiga mayowe. Alifikiri jambo fulani lilikuwa limetukia. Naye huyu hapa akikung'uta mashuka kitandani, alikuwa ndiyo kwanza aamke. Kile kivimbe kilikuwa kimetoweka, hawangeweza kukipata. Alikuwa akiyakung'uta mashuka, akijaribu kukitafuta. Basi wote wawili wakaja mkutanoni kutoa ushuhuda mbele ya watu kama elfu tano. Nini kilitukia? Malaika wa Bwana. Mnaona?

262 Sasa, kumbukeni, Danieli aliomba, na ilikuwa siku ishirini na moja kabla Malaika hajamfikia. Ni wangapi wanaojua hilo? Basi wakati Malaika wa Bwana alipotangaza baraka hiyo, vipi kama alikuwa amekata tamaa? Shetani angeingia moja kwa moja. Lakini alishikilia moja kwa moja.

263 Naye akapitia kwenye ujirani asubuhi hiyo. Anajua mahali unapoishi, yote kukuhusu. Kama anakujua hapa, anajua mahali ulipo. Anapokupa baraka, ataithibitisha, kama tu utadumu nayo. Alipitia kwenye ujirani, na kuwaponya hao wanawake wawili, akienda mahali pengine. Yeye ni Mungu. Yeye si ni wa ajabu? Ni wa ajabu sana.

264 Sasa, nafikiri kwamba...hebu...nafikiri lingekuwa ni jambo jema kama tungeninii...kama ningeweza kuwaulizeni swali. Niliwaombea, hivi karibuni nitakuwa kwenye huduma za kimishenari huko Afrika na India, ambapo wachawi na pepo na kila kitu. Mtaniombea? Je, mtakuwa mkiniombea? Asanteni. *Hata Twonane*.

Hata twonane! hata twonane!
Hata twonane miguuni pa Yesu;
Hata twonane! hata twonane!
Mungu awe nanyi hata twonane tena.

265 Mtaniombea, sasa? Mngefanya hivyo? Sasa, hebu sote tufunge tu macho yetu, tuinue mikono yetu, na tuuimbe. Mpiga kinanda, tupe sauti, nilianza kwa sauti ya chini kidogo, tupe sauti ya *Hata Twonane*.

266 Na sasa, *Hata Twonane*. Na kama hatutaonana tena mpaka upande wa pili wa mto, kumbukeni, nimewaambia ukweli. Nitakuwa Kule pamoja na ushuhuda uo huo. Ninatumaini ya kwamba kama sitawaona tena upande huu, wa Nchi, nitawaona Kule. Lakini nikitumaini nitaweza kuwaona tena hapa. Hata tutakapoonana, Mungu awe pamoja nanyi. Vema, sote kwa pamoja sasa.

Hata twonane! hata twonane!

62-0701 Kuvaa Silaha Zote Za Mungu
National Guard Armory
Santa Maria, California Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org